


# KITENDAWILI

 Asante, ndugu. Asante. Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi. Na huku vichwa vyetu vimeinamishwa, sijui ni wangapi wangetaka kukumbukwa katika maombi, acheni tu ijulikane kwa wewe kuinua mkono wako.

<sup>2</sup> Baba yetu wa Mbinguni, kwa unyenyekevu twaja Kwako, Bwana, tukikiri kwamba hatustahili kuja. Bali kwa sababu kwamba Yesu ametutengenezea njia na amelipa gharama, kwa hiyo, tunaweza kuja kwa ujasiri kwenye Kiti cha neema, katika wakati wa haja. Na sasa, Bwana, kwa vile tupo hapa kuiwasilisha Injili, utajiri unaoweza kutafutika wa Kristo, tunakuhitaji Wewe, Bwana.

<sup>3</sup> Na huenda kukawa na mtu anayeketi hapa, Baba, ambaye Wewe unajaribu kumfundisha kwa njia kuu, ili Wewe uweze kuwatuma mahali fulani, kwenye misheni kubwa ambayo umekusudia Wewe. Ninaomba, Baba, kwamba kama ndivyo ilivyo, kwamba usiku wa leo, kwamba, kusudi Lako litatimizwa. Na utusaidie wakati tunapojikabidhi Kwako kwa ajili ya utumishi.

<sup>4</sup> Sasa, Wewe uliiona mikono yote, na ungali unaangalia ile iliyo juu. Wewe unajua kinachohitajika. Nami naomba ya kwamba utakitimiza, Baba. Ninatoa maombi yangu pamoja na maombi yao, na shauku zao na shauku zangu, juu ya Madhabahu ya dhahabu ambapo dhahabu yetu imewekwa usiku wa leo. Katika Jina la Bwana Yesu, tunaomba ya kwamba Wewe utatumegea, sisi, Mkate wa Uzima, kutoka kwenye Neno Lako. Amina.

Mwaweza kuketi.

<sup>5</sup> Ninasikitika kwa kuchelewa tu kidogo, ila tu nilifahamu kwamba usiku wa leo ilikuwa i—imechelewa tu kidogo, ibada ilikuwa inaendelea kukawia kidogo. Nasi tutafidia hiyo, na kutoka upesi tu iwezekanavyo. Sasa tunataka kulikaribia Neno, usiku wa leo, na kwa yote yaliyokuwamo ndani yetu.

<sup>6</sup> Ninajua mpo hapa, ninyi, baadhi ya hawa waimbaji wazuri mimi... Mel Johnson, mmoja wao, ambaye ninajua ameketi hapa. Nimemwomba atuimbie, sisi, ule wimbo ambao siwezi kabisa kuusahau. Daima ninauvumisha, kuhusu, “machozi yalitiririka chini.” Na—naupenda huo. Nami nafikiri ataimba kwenye kiamshakinywa cha Wafanyabiashara, ama mahali fulani, kwa ajili yetu.

<sup>7</sup> Jim, nataka uwe na hakika na uniletee huo. Na kama una kanda ndogo, uniwekee huo katika hiyo, maalum, yamkini

watoto wangu wanataka kuusikia. Wakati ninapodhoofika kidogo, na—na—nausikia huo, hunifanya kujisikia vizuri, kusikia uimbaji mzuri. Na, Billy, ninaenda ofisini kule chini, naye daima anazo hizo kanda za uimbaji zikicheza wakati wote, nami nafikiri kidogo inamsaidia.

<sup>8</sup> Mnajua, kuna kitu fulani kuhusu wimbo, kilicho na nguvu ndani yake. Sote tunajua hilo. Tuna—tunatambua hilo. Mnaona? Hilo ni, hebu liangalieni jeshi, wanapoimba nyimbo na kucheza muziki. Mnajua jinsi ya kuendea vita, katika jeshi la Mungu, kwanza ni kwa muziki? Waimbaji walilitangulia lile sanduku, wakishangilia na kuimba; ndipo sanduku likafuata; halafu vita. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, hiyo ndiyo njia sahihi ya kuliendea.

<sup>9</sup> Na hiyo ndiyo sababu tunakuja kwenye ibada usiku. Tunafanya nini? Kuimba nyimbo za Bwana; na halafu lile Sanduku, Neno, kusoma Neno; na kisha vita, ndipo tu—tuko ndani. Kwa hiyo bendera kuu zinapepea, usiku wa leo; Jina la Yesu Kristo, Bwana Mungu apate kuinuliwa, adui atimuliwe mbio.

<sup>10</sup> Pia, Mungu, pata ushindi usiku wa leo, na uziokoe nafsi, waponye wagonjwa na wanaoteseka; wafanye wale, waliochoka na kuinama chini, kuinua vichwa vyao na kushangilia, apate utukufu mkuu kwake Mwenyewe. Kwa kuwa tunaomba haya katika Jina la Bwana Yesu.

<sup>11</sup> Ninawatakeni mfungue, usiku wa leo, pamoja nami, kama una Biblia yako, na wakati mwingine watu hutia alama fungu dogo ambalo wahudumu wanazungumzia. Ilikuwa kwamba ningeweza kuwazia hivi upesi sana, bila hata kuviandika. Lakini baada tu ya mimi kupita umri wa miaka ishirini na mitano, mbona, miezi michache iliyopita, namaanisha mara ya pili, na kwa hiyo inaifanya ngumu kidogo kwangu kukumbuka. Ninayo makovu mengi kutoka vitani. Na kadiri tunavyozidi kuzeeka, kabisa hatuwazii jinsi tulivyo zoea kuwaza, nami nina... Ninapoyaangalia Maandiko na kuona, basi ninakumbuka ni somo gani.

<sup>12</sup> Hebu tufungue Yoshua, mlango wa 10, tuanze kusoma kwenye kifungu cha 12.

*Ndipo Yoshua akanena na BWANA katika siku hiyo ambayo BWANA aliwatoa Waamori mbele ya wana wa Israeli; akasema mbele ya macho ya Israeli, Wewe Jua, simama kimya juu ya Gibeoni, na... Mwezi; simama juu ya bonde la Aiyaloni.*

*Ndipo jua likasimama na mwezi ukatulua, hata hilo taifa lilipokuwa limekwisha kujipatiliza juu ya adui zao. Hayo, je! Hayakuandikwa ndani ya kitabu cha Yashari? Basi jua likasimama kimya katikati ya mbingu, wala halikufanya haraka kuchwa kama muda wa siku nzima.*

*Haikuwapo siku nyingine mfano wa siku hiyo katika siku zilizotangulia mbele yake wala katika siku zilizoandama baada yake, hata ikawa yeye BWANA kuisikia sauti ya binadamu; kwa kuwa BWANA alipiga vita kwa ajili ya Israeli.*

<sup>13</sup> Bwana na aongeze baraka Zake kwenye kusomwa kwa Neno Lake. Ninataka kuchukua somo kutoka hapo kwa yapata dakika thelathini, kama ninaweza kulishikilia kwenye hilo: Kitendawili. Kutumia tu neno hilo moja: *Kitendawili*.

<sup>14</sup> Sasa kulingana na Webster, *kitendawili* ni “kitu kinachoonekana hakiaminiki, bali ni cha kweli,” kwa hiyo kitendawili basi kingekuwa ni kama mwujiza. Kitendawili ni wakati kitu ambacho—ambacho kinaonekana kana kwamba kisingewezekana kabisa, ma—maarifa ya akili ya binadamu; kwa jumla hakiaminiki, bali hata hivyo kinathibitika kuwa ni kweli. Sasa, mwujiza ungekuwa ni kitu kile kile, kwa maana mwujiza hauwezi kuelezewa. Mwujiza ni kitu kinachotendeka, wala huwezi kukieleza, hicho kinakifanya kuwa ni kitendawili. Hakiaminiki, bali hata hivyo ni kweli.

<sup>15</sup> Sasa, watu leo hii, watu wengi wa kisasa, wanaamini ya kwamba siku za miujiza zimepita. Hawaamini kuna kitu kama mwu—mwujiza. Lakini, hata hivyo, ninaamini ya kwamba ulimwengu umejaa miujiza. Ninaamini kitendawili ni kila mara.

<sup>16</sup> Kwa mfano, ninaamini ya kwamba kila mshiriki wa Mwili wa Kristo aliyezaliwa upya wenyewe ni kitendawili. Ninaamini kila mmoja wenu Wamethodisti na Wapresbiteri na Lutheri, ambao kamwe hamkuwa mmepata tukio la ubatizo wa Roho Mtakatifu, mlikuwa kwenye kanisa fulani la kawaida ambalo halikuamini katika Kuzaliwa upya kwa kweli, na sasa mmeupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ni mfano mkamilifu wa kitendawili. Kwa sababu, jambo fulani lilikufanyikia, ambalo liliubadilisha utu wako wote, na mtu yeyote angeweza kuangalia hilo na kujua kitendawili ni kitu gani: mwujiza.

<sup>17</sup> Isipokuwa hilo litendeke, huwezi kuwa Mkristo. Hapana budi pawe na kitendawili, ili uweze kuwa Mkristo. Maana, hakuna mtu anayeweza—anayeweza kubadili roho ndani ya mwanadamu, na kumpa Kuzaliwa kupya, nje ya Mungu. Mungu pekee Ndiye tu anayeweza kulifanya. Na ni mwujiza jinsi ambavyo Mungu anaweza kuchukua mawazo ya mwanadamu, na njia zake, na maisha yake, na kila kitu, na kuyabadilisha kutoka kwenye kile yalichokuwa, kufikia kile yanachoweza kuwa, kile Yeye anachoweza kuyafanya.

<sup>18</sup> Kwa mfano, siku chache zilizopita, niliitwa ndani kwenye tu—tukio fulani, ama kitu ki—kidogo kilichokuwa kinaendelea. Kulikuwako na kijana mwanamume mzuri sana, mvulana mzuri sana, alikuwa akiambatana na msichana mdogo, msichana mdogo mzuri sana kutoka kwenye familia nzuri. Ndipo mvulana

huyu, mara ghafla, akatokea na wazo la namna fulani, na akaondoka tu. Alimfanyia jambo baya maskini msichana huyo, na kiasi kwamba alimwahidi kufanya jambo fulani na halafu hakulifanya. Basi badala ya kumjia msichana huyo na kuomba msamaha, kama mwu—mwungwana anavyopaswa kufanya, yeye, kabisa haikuwa ndani yake kufanya hivyo.

<sup>19</sup> Ndipo baba na mama yake wakaniita jukwaani, na kusema, “Tungetaka kujua shida ya mvulana wetu.”

<sup>20</sup> Sasa, si rahisi kufanya wakati mwingine, bali huna budi kuwa mkweli na mwaminifu. Kwa hiyo, mvulana huyo alikuwa ni Mkristo, kuhusu kuwa mwaminio. Alikuwa ametubu na alikuwa amebatizwa, naye alikuwa na mahali pake miongoni mwa waaminio, bali hata hivyo hakuwa amepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, haidhuru alidhani amepokea kiasi gani.

<sup>21</sup> Wewe kufikiria unaye, na kuwa Naye, ni vitu viwili tofauti. Huenda ukaweza kujaribu kusema unaye, na huenda unaweza kuonyesha baadhi ya ushahidi wa mhemuko fulani; bali isipokuwa maisha yako yanathibitisha kile unachokiri kuwa nacho, bado hunaye Huyo. Haidhuru ni mihemuko mingapi, unaruka kiasi gani, kukimbia, misisimko, kunena kwa lugha, ama kupaza sauti, ama chochote unachoweza kuliwekea; ambalo ni sawa, ninaamini katika hayo yote, pia; bali isipokuwa maisha yako yaambatane na ushuhuda wako, basi hunaye Huyo. Maana, tunda la Roho huthibitisha ulicho wewe, kama tu vile tunda la mti wowote huonyesha kwamba ni upi. Yesu alisema, “Kwa tunda lao mtawatambua.”

<sup>22</sup> Sasa, wazazi wa jamaa huyu kijana. Mama yake ni Mjerumani. Sio kuwashutumu Wajerumani, lakini kuna tabia katika familia hiyo. Na, hiyo ni kusema, wao wataketi kitako tu, nawe waweza kuzungumza nao, nao wataku kodolea macho tu. Wana ninii... Dada yake msichana huyu, mama yake mvulana huyu, dada yake. Nimepitia barabara hiyo, asubuhi nyingi, naye msichana huyu atakuwa ameketi nje uani, nami ningesema, “Habari za asubuhi, kwako.” Angeniangalia tu. Nami ningesimama, na ningesema, “Hakika ni asubuhi njema.” Angesimama tu, akuangalie moja kwa moja; mwanamke mwenye akili. Ndipo ningesema, “Njoo ukatutembelee wakati mmoja.” Angesimama tu na kuangalia. Vema, ndugu zake wako hivyo, baba na mama wako hivyo.

<sup>23</sup> Sasa baba ya mvulana huyo, ni Mwairishi halisi, mwenye moyo mzito, na mwenye hasira, hamaki kuu. Hiyo ni familia yake yote namna hiyo, isipokuwa mwingine mmoja kutoka kwenye familia hiyo, aliyeongoka. Sasa katika jambo hili, mvulana huyu...

<sup>24</sup> Baba huyu na mama, wote wawili ni Wakristo, waliojazwa na Roho Mtakatifu, nao wamemlea kijana mwanamume huyu katika njia ya Bwana. Na sasa kijana mwanamume huyo ana

umri wa kadiri ya miaka kumi na saba ama kumi na nane, kitu karibu hapo, mtoto mzuri sana, na yeye—yeye amekuwa mvulana kielelezo halisi nyumbani, mtoto mzuri. Naye ana kaka ambaye ni kinyume chake kabisa.

<sup>25</sup> Lakini hao wasichana, familia ya mama, wanaishi karibu na... kanisa zuri. Lakini unafikiri wangewahi kuja kule? La. Nao wanajua Hilo ni sahihi, bali haiko ndani yao kabisa ku—kuomba msamaha ama kuomba kusamehewa. Kamwe hawatafanya hivyo. Haiko ndani yao kabisa.

<sup>26</sup> Sasa zile jeni katika baba na mama wa mvulana huyu, haijalishi wameongoka kiasi gani, zingali zinabaki mwili ambao zimechanganywa zikawa mvulana huyu. Kwa hiyo, mvulana huyu ana kinyongo ndani yake, kama tu kutoka kwenye familia ya mama yake, nao hawasamehe, hawataomba msamaha, na hapo ndipo mvulana huyo anaposimama.

<sup>27</sup> Sasa, nikamwambia baba yake, “Haijalishi umemlea jinsi gani...” Nikasema, “Sasa iangalie wewe mwenyewe, kutoka kwenye familia yako: wote, walevi, na—na kupigana, na kurushiana risasi, na kukatana, na kadhalika.”

<sup>28</sup> “Sasa iangalie familia yako,” kwa mama yake. “Hao ni kundi la watu, wanaketi tu hapo na hawataongea, wapweke kabisa, na kadhalika, hawana kicho kwa dini. Lakini,” nikasema, “sio wewe. Wewe ndiwe pekee miongoni mwa dada zako wote na kaka, nawe ni mwema, mkarimu, na mwenye kusamehe. Ni kitu gani kinachosababisha hilo? Nawe ni ukoo, sehemu ya ukoo huo wa familia, hata hivyo umempokea Roho Mtakatifu. Hilo ndilo jambo lililokufanya mpole na wa kupendeza. Si watu wako tena, ni Kristo wako aishiye ndani yako.”

<sup>29</sup> Nikamwambia mvulana huyo, “Angalia familia yako, karibu wote ni walevi, na kadhalika.” Nikasema, “Na jinsi walivyo wenye mioyo mizito, na—na wenye hasira kali na hamaki kuu, bali sivyo ulivyo wewe. Wewe ni mkarimu, mwenye huruma. Ni kitu gani? Roho Mtakatifu. Wewe si kile ulicho tena; ni Kristo ndani yako.” Nikasema, “Sasa jambo lilo hilo halina budi kutukia kwa mwanao.”

<sup>30</sup> Ndipo huyo baba akasimama na kusema, “Mwanangu alienda madhabahuni. Alibatizwa kwa njia sahihi, katika Jina la Yesu Kristo, na ubatizo wa maji kwenye kidimbwi.” Kasema, “Najua mwanangu amemjia Kristo.”

<sup>31</sup> Nikasema, “Hilo laweza likawa ni sawa, matendo yote ya nje. Huenda akatambulishwa kama mwaminio pamoja na waaminio. Bali mpaka atakapoongoka, kuzaliwa mara ya pili, ningemshauri kijana mwanamume huyo kamwe asimwoe mwanamke. Atamtengenezea Kuzimu duniani, mpaka Roho huyo wa Kristo mpole, wa kupendeza, mwenye huruma atakapoingia ndani. Ndipo hiyo yenyewe itakuwa ni kitendawili, kuchukua tabia yenyewe ya mvulana ambaye amezaliwa kati

ya baba na mama. Na hata hivyo, katika akili zake, anajaribu awezavyo kushinda hilo. Hawezi kushinda. Kamwe hatashinda hilo. Kristo hana budi kulishinda. Anapomruhusu Kristo ndani, basi tayari ameshinda basi. Itakuwa ni kitendawili kikamilifu, wakati mtu amezaliwa kwa Roho wa Mungu.

<sup>32</sup> Nimewaona wakosoaji wakisimama kando na kudhihaki, na kufanya yasiyofaa, juu ya uamsho wa Roho Mtakatifu. Ndipo baada ya kitambo kidogo, Mungu anamshika mtu huyo huyo na kumbadilisha, naye huyu hapa anasimama mimbarani akihubiri jambo lile lile ambalo wakati mmoja alilichukia. Ni kitendawili, jinsi ambavyo Mungu anaweza kumchukua asiyeamini na kufanya mwaminio kutoka kwake.

<sup>33</sup> Sasa sijui, kama mtu anafikiri kwamba miujiza imepita, sijui ni aina gani ya dawa ya kisayansi ungaliweza kumpa mtu kama huyo kubadilisha tabia hiyo ndani yao, kuondoa hiyo chuki na kijicho na ugomvi, vitoke? Hukuna mtu anayeweza kulielezea. Bali ni kitendawili, kwa sababu ni mwujiza wa Mungu. Wakati mtu anapobadilishwa kutoka kwa mtu aliye, akawa kiumbe kipya katika Kristo Yesu, anakuwa kiumbe kipya. Yeye si kile alichokuwa tena. Yeye kabisa ni kiumbe kipya ndani ya Kristo.

<sup>34</sup> Ulimwengu huu wenyewe, tunaishi, ni kitendawili kabisa, jinsi ulivyoubwa. Tunaona, katika Waebrania mlango wa 11 na kifungu cha 3, kwamba, “Ulimwengu uliunganishwa pamoja kwa Neno la Mungu.” Mungu alipata wapi nyenzo za kuufanya ulimwengu huu? Alifanyaje jambo hilo? Biblia inasema ya kwamba “ulifanywa na kuunganishwa pamoja.” Miundo yake yote na sehemu yake ziliunganishwa pamoja kwa Neno la Mungu. Kama hicho si kitendawili, sijui kiko wapi. Tungeweza kutoa wapi na kusema Yeye alipata hizo nyenzo, wakati hapakuwapo na nyenzo? Ilimbidi azinene ziwepo. Ni kitendawili, kwamba ulimwengu huu uko hapa usiku wa leo.

<sup>35</sup> Jambo jingine, ni kitendawili jinsi unavyodumu kwenye mzingo wake, ukining’inia hewani. Unawezaje kuning’inia pale kwenye mahali hapo pamoja, ukizunguka kasi *hivi*, yapata maili elfu moja na mia moja kwa saa? Maili elfu ishirini na nne ama ishirini na tano mzunguko, na unazunguka kila saa ishirini na nne, kikamilifu sana hauptotezi hata sekunde moja. Unazunguka kikamilifu sana, zaidi ya kuliko karibu. . . Zaidi ya maili elfu moja kwa saa, unazunguka namna *hii*, ukining’inia hewani. Kama ungepanda juu ama kushuka, lolote lile, mbona, jamani, unge—ungepatiza mfumo wote wa mfumo wa Mungu wa jua. Nao unazungukia kwenye ikweta, kuzunguka huo mzingo mara nyingi, katika muda wa mwaka mmoja, bila kukosea, majira vivyo hivyo hasa.

<sup>36</sup> Niambi ni kitu gani kinachoushikilia huko juu, ni kitu gani kinachouzungusha kikamilifu hivi katika wakati. Unaweza kupata saa ya mkono; sijui unaweza kununua moja kwa bei gani,

dola elfu moja; nayo hiyo saa, katika kipindi cha mwezi mmoja, itapokeza dakika kadhaa. Hawana kitu kinachoweza kufanya kazi kikamilifu sana, bali hata hivyo ulimwengu huu huzunguka kikamilifu. Kwa nini? Ni Mungu anayefanya hilo. Ni kitendawili. Mungu aliuamuru kufanya hivyo, nao unafanya hivyo.

<sup>37</sup> Vipi kuhusu mwezi? Ingawa uko maili milioni kadha kutoka duniani, na hata hivyo hu—hudhibiti kujaa na kupwa kwa maji duniani. Umbali wa mamilioni ya maili, athari yake, ya kusimama mahali pake angani. Kusimama kwenye mzingo wake, inaathiri dunia. Kila sayari huathiri nyingine, kwa kudumu mahali pake.

<sup>38</sup> Loo, ni mahubiri ya jinsi gani ningaliweza kuchukua kutoka hapa, somo! Jinsi ambavyo kila mmoja wa viumbe vya Mungu angedumu mahali pake, kingeshawishi mwenziwe. Lakini tunaondoka kwenye maskini hamaki fulani mahali fulani, na kuunda dhehebu na kujitenga wenyewe, kana kwamba hatuna imani, na ndipo tunauvuruga mfumo wote wa Ukristo. Kama kila mtu angedumu mahali pake, ingekuwa ni kitendawili cha Mungu, kuona jinsi ambavyo Mungu angewaleta Wapresbiteri, Walutheri, Wabaptisti, Wamethodisti, Wakatoliki, na wote pamoja. Kama tungerudi kwenye Neno la Mungu, ingekuwa ni kitendawili halisi. Halafu basi kanisa zima lingeweza kukubaliana, sio juu ya kanuni zenu za imani na kadhalika, bali juu ya Neno, jinsi Hilo lilivyoandikwa. Kwa sababu, “Si la kujifasiria apendavyo mtu mwenyewe,” yasema Maandiko.

<sup>39</sup> Jinsi ambavyo huo mwezi huathiri dunia! Hapa si muda mrefu uliopita, rafiki yangu, jirani yangu, alikuwa akichimba mashimo kwa ajili ya visima vya mafuta, huko chini katika jimbo la Kentucky. Ndipo wakati huo mwezi unapoanza kuchomoza kule, maji kujaa huja kote kupitia ardhini. Maji hayo ya chumvi, huko chini katika shimo ambapo walichimba, yatapanda juu wakati huo mwezi unapochomoza. Haijalishi, kama liko chini mamia ya futi chini ya sakafu ya ninii... ama juu ya nchi hapa. Yanashuka chini kwa futi mia kadhaa, hata hivyo, wakati huo mwezi unapogeuka, hayo maji hupanda kukutana nao. Yalipanda.

<sup>40</sup> Huwezi kuficha chochote, wakati Mungu amekiamuru. Hakina budi kumtii Mungu, wakati Mungu anapotoa amri Yake. Hiyo ndiyo sababu ninajua Yeye atakuwa na “kanisa lisilo na waa ama lisilo na kunyanzi,” Mungu ameliyamuru hivyo. Italibidi kutii. Mungu atakuwa nalo, maana Neno la Mungu limesema hivyo.

<sup>41</sup> Jinsi ambavyo maji kujaa na kupwa, mwezi, na kila kitu, huathiri matendo ya duniani! Hebu chukua. . .

<sup>42</sup> Tunaona nyota ikivurumisha, tunaiita nyota. Hiyo si nyota ikivurumisha. Ni nuru. Hakika, tunajua hilo, bali tunaiita nyota.

Hiyo nyota isingeweza kusogea umbali huo. Kama nyota moja ingaliondoka kwenye mzingo wake, labda ingeathiri kila kitu katika mkondo huo, ulimwenguni kote. Ingeathiri. Ingetatiza. Kila kitu hakina budi kukaa mahali pake, kusudi idumishe mfumo wa Mungu katika mwendeleo.

<sup>43</sup> Vivyo hivyo hatuna budi kudumu mahali petu, hatuna budi kukaa kama wana na binti za Mungu. Kama hatukuanguka kule nyuma, kitu hicho kingalikuwa kinazunguka, kusingekuwako na mauti wala chochote kingine. Bali Mungu na ashukuriwe, kitendawili kinakuja, wakati Mungu Mwenyewe ataurudisha mahali pake ambapo unapaswa kuwa. Naam, kitendawili.

<sup>44</sup> Mtu asiyeamini katika—katika kitendawili, wala haamini katika miujiza, ungewezaje kuitetea akili yako, na kuangalia moja kwa moja kwenye mambo usiyoweza kuelezea? Haiwezekani kabisa kwa mtu yeyote kuelezea jinsi ambavyo ulimwengu huo unavyoweza kujizungusha na kuweka wakati mkamilifu, na (hata) mfumo wote wa jua na mambo hayo, na jinsi ambavyo mwezi unaweza kuiathiri dunia. Basi ni mambo mengine mangapi tungeweza kusimulia!

<sup>45</sup> Jinsi ambavyo u—utomvu kwenye msimu wa majani kupukutika mwakani utakavyoshuka kuingia kwenye mzizi wa mti, pasipo na akili yoyote ya kuushusha mle, kuirudisha kwenye msimu wa kuchipusha wa mwaka, pamoja na uhai mpya, mbona, ni kitendawili. Hakuna anayeweza kulielezea. Hatujui jinsi linavyotendeka. Bali Mungu analifanya, kwa hiyo ni kitendawili, daima. Ni siri jinsi Mungu anavyofanya hivyo. Tunaliangalia sana hata linakuwa ni la kawaida sana. Tunaangalia kupitia juu yake.

<sup>46</sup> Na hiyo ndiyo shida yetu (sisi) watu wa Kipentekoste. Tumemwona Mungu akitenda vitendawili vingi sana hata inakuwa tu ni mara chache ambapo hata tunaliwazia. Laiti tungalisimama tu kwa dakika moja na kutafakari! Mungu yuko kila mahali. Mungu a—anatenda kazi. Na saa Yake ya kale inapiga kote hukuu, mpaka hatimaye itaingia moja kwa moja katika Umilele, kwa sababu Mungu ameiahidi kufanya hivyo. Sasa tunajua kwamba kuna kitendawili.

<sup>47</sup> Sasa, huko nyuma katika siku za Nuhu, kabla mvua haijaja, na gharika. Lilikuwa ni jambo gu—gumu sana kwa Nuhu, katika ule wakati mkuu wa kiakili alimoishi, kujaribu kuwaambia watu, kwa Neno la Mungu, kwamba ilikuwa inaenda kunyesha. Sasa ingekuwa, bila shaka, kwamba haikukidhi si—sifa za utafiti wao wa sayansi. Hapakuwapo na mvua angani. Lakini, mnaona, Nuhu alisema kutakuwako na mvua kwa sababu Mungu alisema kutakuwako na mvua. Ndipo Nuhu, kwa imani, kabla ya mvua kuja, alisema ingekuwako.

<sup>48</sup> Hiyo ndiyo sababu tunasema jambo lile lile. Kwamba, wao wanasema, “Mbona, Yesu, wao walisema Yeye alikuwa anakuja



muda mrefu uliopita. Mamia ya miaka iliyopita, walidai Yeye alikuwa anakuja. Mitume walisema hivyo; labda kizazi chao.” Hilo halilikomeshi hata kidogo. Tungali tunajua Yeye yuaja. Itakuwaje? Sijui. Lakini Mungu atamtuma. Aliahidi kumtuma, nami najua Yeye atakuwa hapa.

<sup>49</sup> Sasa, Nuhu angeweza tu kusema, “Mungu alisema hivyo.” Lakini, mnaona, basi, hata hivyo, halikutosheleza idhini yao ya kisayansi kwenye siku hiyo. Lakini wakati ulipowadia kwa Neno kutimizwa, ilinyesha, haidhuru. Hicho kilikuwa ni kitendawili kwelikweli katika siku hiyo, kuwazia ya kwamba mvua ingeweza kuja kutoka angani, ambako hamna mvua.

<sup>50</sup> Lakini kama Mungu akichukuliwa kwenye Neno Lake, Yeye anaweza kutenda, kufanya kitendawili. Anaweza kufanya mwujiza. Na mtu yeyote aliyezaliwa kwa Roho yuyo huyo anayefanya miujiza, mbona, ni jambo rahisi kwake kuamini miujiza, kwa sababu yeye ni sehemu ya Mungu. Amina.

<sup>51</sup> Mwana na binti wa Mungu; sio kwa dhehebu, sio kwa kanuni ya imani, sio kwa kupeana mkono; bali kwa kuzaliwa, kwamba umekufa kwa akili zako mwenyewe, na umezaliwa kwa Roho wa Mungu. Na wewe ni kitendawili, wewe mwenyewe, jinsi ambavyo umebadilishwa kutoka mautini kuingia Uzimani. Kutoka kwenye kiini cha utu wako wa ndani kabisa kuna kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Ni kitendawili.

<sup>52</sup> Mungu hunena Neno Lake, watoto Wake wanaliamini na Mungu. Sayansi haiwezi kuthibitisha jinsi inavyoweza kufanyika; hawajui chochote kulihusu. Bali watoto wanaliamini, kwa vyovyote vile, na ndipo Mungu anafanya kitendawili, analitimiza. Analitimiza, kwa sababu Neno Lake lililounena ulimwengu ukawepo, linaweza kuleta, linaweza kufanya kila neno, Yeye alilowahi kuahidi, litimie.

<sup>53</sup> Hiyo ndiyo sababu Ibrahimu hakusita kwenye ahadi ya Mungu, kwa kutokuamini, bali alishawishika kabisa ya kwamba Yeye aliweza kufanya na kudumisha kile Yeye alichosema angefanya. Hakusita kwenye ahadi ya Mungu, akiwa na umri wa miaka mia moja, naye Sara tisini, kumpata mtoto huyu. Kwa sababu kwamba alijua ya kwamba Mungu angeweza kufanya na (kufanya) afanye kitendawili kitukie juu ya jambo fulani, mwujiza ufanyike, na Yeye akaufanya.

<sup>54</sup> Wale wana wa Kiebrania. Sasa ungeifanyaje sayansi iamini leo hii ya kwamba mtu angeweza kuingia katika tanuru? Loo, ningehofia kusema ilikuwa na joto la Farenhaiti ngapi; bali wangeweza kuingia kwenye ile tanuru huko nyuma, katika Kitabu cha—cha Danieli, na kukaa kwenye tanuru hiyo mpaka wakadhandia kwamba yeye, wote walikuwa wameteketezwa wakawa majivu. Ambalo, hata mtu huyo, lile jeshi kubwa la askari, watu wakubwa mno waliojongelea pale ku—kuwatupa kwenye tanuru, hao watu walioingia mle waliangamia, kwa joto

kali mno la tanuru dhidi yao. Nao wakaanguka kwenye tanuru, nao walikuwa mle ndani wakati huu wote, kisha wakatokea bila hata harufu ya moto juu yao.

<sup>55</sup> Mungu, akifanya mwujiza! Hicho kilikuwa ni kitendawili halisi, cha nguvu za kuhifadhi za Mungu, dhidi ya adui yeyote, wakati mtu akiwa tayari kukubali Mungu ni kweli. Naye Mungu hutimiza Neno Lake na kuwaheshimu wale wanaomwamini Yeye. Hakika ninaamini katika kitendawili.

<sup>56</sup> Yoshua, yule shujaa hodari ndiyo kwanza nisome habari zake, dakika chache zililizopita, katika Kitabu cha Yoshua, mlango wa 10. Angalia, Yoshua alikuwa ra—rafiki wa Mungu. Alikuwa ni askari, je—jemadari, naye alitokea chini ya ushawishi wa nabii, Musa. Naye Musa alikuwa ameondolewa, naye Yoshua akaamuriwa kuwapeleka wale watoto kwenye nchi ya ahadi, na kuigawa nchi. Kule kutotii kwa watoto; na Musa alikuwa amengojea kuwa mzee, na kwa hiyo Yoshua akaja kupachukua mahali pa Musa, kuwa jemadari wa Mungu.

<sup>57</sup> Basi Bwana akanena naye, na kusema, “Kama nilivyokuwa pamoja na Musa, ndivyo nitakavyokuwa pamoja nawe.” Hilo ni zuri vya kutosha kwa Yoshua. Kasema, “Uwe hodari na ushujaa mwingi, kwa kuwa Bwana Mungu wako yu pamoja nawe popote uendapo. Na kila mahali zitakapokanyaga nyayo za miguu yenu, hapo nimewapa ninyi.” Basi, nyayo za miguu zinamaanisha umilikaji. Nchi yote ilikuwa ni mali yao. Ilikuwa ni ahadi.

<sup>58</sup> Mapema kabisa kabla halijatukia, wakati alipokuja pale chini pamoja na Kalebu na wapelelezi hao wengine, nao wakaona ule upinzani mkuu, wale Waamaleki, na—na Waperizi, na Wahiti, na kadhalika, wote wamezingirwa ndani, na kule Yeriko kungeweza kukimbia mbio za magari ya farasi juu ya—ya mahali hapo, na ni watu wakubwa mno wenye nguvu. Hao, baadhi ya wa—wasioamini miongoni mwao, walisema, “Mbona, tunaonekana kama panzi karibu nao.”

<sup>59</sup> Bali Kalebu akasema, na Yoshua, “Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka.”

<sup>60</sup> Kwa nini? Mungu alisema, “Nimewapa nchi hii.” Haidhuru ni nini upinzani, jinsi ulivyo mkubwa na—na shi—shi—shida zinavyoonekana, hata hivyo Mungu alisema ilikuwa ni yao. Loo! Mungu anaweza kutimiza kile Yeye ameahidi.

<sup>61</sup> Ilikuwa ni kitendawili, kuna kundi dogo la watu, wasio na silaha, karibu hawana, ila zile walizokuwa wameokota jangwani, na ambako walikuwa wamewafukuza watu wengine, labda wakiwa na reki za kale na misumeno, na chochote walichoweza kupata. Kuingia mle na kuwapiga hao watu kabisa, waliokuwa ni majitu. Ilikuwa ni kitendawili. Mungu alijua kwamba walikuwa na ujasiri wa kufanya hilo. Naye akawapa ahadi, nao wakaingia na kufanya yale hasa Mungu aliyowaahidi kufanya.

<sup>62</sup> Siku moja, wakati vita vimepamba moto, wakati wafalme walikuwa wamefanya agano kubwa miongoni mwao na walikuwa wameshuka wakaja dhidi ya Yoshua na wana wa Israeli. Kwamba, Mungu alikuwa amewaahidi nchi hiyo. Naye alikuwa amempiga adui, nao walikuwa misituni na vilimani, wametawanyika kote nyikani kule, ndipo Yoshua akaangalia na akaona jua likishuka. Alijua kama hayo majeshi yangepata nafasi kujibadilisha na—na kurudi tena kwake, mbona, alijua ya kwamba angekuwa na wakati mgumu maradufu na huenda akawapoteza watu zaidi, kama kamwe walipata mahali pa kuungana pamoja.

<sup>63</sup> Hapo ndipo, wahudumu, hapo ndipo tunaposhindiwa. Hapo ndipo kanisa hushindwa. Wakati huu uamsho ambao ndio kwanza tuwe nao, miamsho hii mikubwa iliyoanza kote nchini, wakati tulipowafanya adui kukimbia, ilitupasa kumfanya aendeleo kutoroka. Lakini, jambo ni kwamba, inatubidi kuendea hamaki tu na kadhalika, na harakati kubwa mno za mijengo na “kupata wengi zaidi kwa ajili ya kundi letu,” na kadhalika. Nanyi hao hapo mnakuja, na kujitenga wenyewe na Neno, na kuchukua *hili, lile*, kisha kujenga madhehebu yao zaidi, na kuanzisha kitu kingine. Hivyo ndivyo inavyoenenda daima. Hivyo ndivyo ilivyokuwa katika siku za Luther, Wesley, na Moody, Sankey, Finney, Knox, Calvin, kote kote chini. Imekuwa ni vivyo hivyo. Wanaondoa macho yao kwenye u—uamsho, na kuyaelekeza katika kile wanachoweza kufanya wenyewe.

<sup>64</sup> Bali mnajua kilichotukia? Yoshua hakuwa mtu wa namna hiyo. Alihitaji wakati. Jua lilikuwa likishuka, naye alijua kama adui atawahi kujihami. . . Uamsho ulikuwa umekaribia mwisho wa kumalizika kwake, kama tulivyo leo hii. Alijua kama angengejea mpaka adui ajihami dhidi yake, ingekuwa vigumu kushinda vita hivyo. Mnajua kile alichofanya? Alijua ya kwamba Mungu aliahidi nchi hiyo. Alihitaji muda zaidi. Kwa hiyo jua lilikuwa karibu kutua, ndipo akasema, “Ewe jua, simama kimya.” Amina. Kitendawili, kweli. Ndipo hilo jua likasimama pale siku nzima, na halikusogea; na mwezi juu ya Aiyaloni, kamwe haukusogea, pia.

<sup>65</sup> Kwa sababu, Biblia ilisema hapa, ya kwamba, “Hapakuwapo na wakati hapo kabla, ama baadaye, mfano wake, ambapo Mungu aliisikia sauti ya binadamu.”

Mnasema, “Loo, laiti ningalijua tuliishi tu katika siku hiyo!”

<sup>66</sup> Yesu alisema, katika Marko Mtakatifu 11:24, “Ukiuambia mlima huu, ‘Ng’oka,’ na usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba uliyosema yatatimia, yatakuwa yako yale uliyosema.” Ingali ni neema, na kitendawili, kote mpaka kuufikia wakati wetu. Hakika.

<sup>67</sup> Huo mwezi na jua vilisimama kimya mpaka Yoshua akavipiga na kumaliza vita vyake, pamoja na Israeli, na

kujipatiliza juu ya adui wao. Kwa nini? Ilikuwa kwenye jukumu lao.

<sup>68</sup> Sasa kama ungetoka hapa nje na kusema, “Mlima, ng’oka! Ninataka kuwaonyesha ya kwamba ninaweza kufanya hilo.” Hautang’oka.

<sup>69</sup> Lakini kama liko kwenye jukumu, wakati Mungu amekuamuru kufanya jambo fulani! Kama alivyomwambia Musa, “Mbona unanililia? Nena na hao watoto.”

<sup>70</sup> Watu leo hii wanalia wakati wote, “Bwana, ni nini kinachofuata, ni nini kinachofuata?” Nena tu na usonge mbele! Hiyo ni kweli. Mungu ametuagiza kufanya jambo fulani, hebu na tulifanye. Usisimame huku na kuliwazia, useme, “Inawezekanaje? Vema, *hili* ni lile.” Inaleta tofauti yoyote; kama Mungu alisema ulifanye, lifanye hata hivyo. Yeye angali ni Mungu wa miujiza.

<sup>71</sup> Yoshua, hakika ilikuwa ni kitendawili wakati lile jua liliposimama kimya. Nilikuwa nikizungumza na mwa—mwanasayansi shuleni wakati mmoja, naye alikuwa ni mwalimu wa Biblia. Basi akasema... Nilimrejeshea hili. Nikasema, “Nilifikiri ulisema ya kwamba du—dunia iligeuka, unaona, na—na jua likasimama kimya?” Nikasema, “Vipi kuhusu Biblia ndiyo kwanza utwambie ilikuwa ni kweli? Mungu... Yoshua alisema, ‘Jua, simama kimya.’” Vema, asingeweza kujibu hilo.

<sup>72</sup> Lakini jua lilisimama kimya. Halikusogea hata kidogo, mnaona. Hiyo kweli ni dunia iliyosimama. Na sasa unasema...

Akasema, “Dunia ilisimama.”

<sup>73</sup> Nikasema, “Ulisema, ‘Kama dunia ingalisimama, ingalipoteza nguvu zake za uvutano na kila mtu angeanguka kutoka kwake.’ Sasa utafanya nini?”

<sup>74</sup> Ni kitendawili. Amina. Mungu aliisimamisha dunia nzima isizunguke, amina, kwa sababu mwanadamu alisema, “Simama kimya hapo, mpaka nitakapomaliza kupiga vita hivi.” Hicho ni kitendawili. Amina.

<sup>75</sup> Ilikuwa ni kitendawili wakati majeshi yote ya Israeli yaliposukumwa pembeni, nao walikuwa wanaliogopa jitu kubwa mno la zamani za kale lililosimama pale, jina lake Goliathi. Na hapo majeshi ya Israeli, Sauli aliyefunzwa vizuri, kichwa na mabega yako juu kuliko jeshi lake lote, na huku anatetemeka kwenye buti zake. Hakuna mtu aliyeweza kukabiliana na changamoto ya mtu huyu wa siku hiyo.

<sup>76</sup> Akaja maskini mtoto, mwekundu kwa kuonekana, mwenye mabega yaliyoinama, mwenye uzito wa yapata ratili tisini, huku amejizungushia kipande cha ngozi ya kondoo namna hiyo. Akasema, “Aibu kwa jeshi hili la Mungu aliye hai; kusimama hapa na kumwacha huyo Mfilisti asiyetahiriwa kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai.”

<sup>77</sup> Wakati neno lilipomfikia Sauli, Sauli alisema, “Wewe si kitu ila kijana, na yeye ni askari wa vita tangu ujana wake. Na wewe ni mtoto, hebu angalia jinsi alivyo. Mbona, usingeweza kumkabili.”

<sup>78</sup> Lakini yeye alichukua nini? Hakuchukua mkuki, kamwe hakuchukua upanga, bali alichukua kombeo. Na ni mahali pamoja tu angaliweza kupigwa jitu hilo, hapo palikuwa moja kwa moja kwenye kipaji cha uso, ambapo silaha yake ilishuka juu ya uso wake kuyaficha macho yake. Nalo jiwe hilo, na masafa marefu kutoka kwenye mkuki huo wa sindano wenye urefu wa futi kumi na nne aliokuwa nao mkononi mwake; ulikuwa mrefu kabisa jinsi ulivyokuwa, ungeweza kumtwaa maskini Daudi na kumfanyia chochote, na kumning’iniza mtini, kama alivyotishia kufanya, na kuwaacha ndege waule mzoga wake.

<sup>79</sup> Lakini ni jambo gani lililotukia? Kulikuwako na kitendawili, wakati Mungu alipomchukua maskini mtu mwekundu asiyevutia macho, hata kidogo, si hata askari aliyefunzwa, mtoto tu aliyekuwa na imani Kwake, na kuiaibisha nchi nzima. Mungu alifanya hilo kwa kitendawili.

<sup>80</sup> Amina! Yeye angali ni Mungu, usiku wa leo, wa kitendawili, kama tu Yeye alivyokuwa wakati huo.

<sup>81</sup> Alilivuruga jeshi zima. Waliona hilo, ndipo wakaanza kukimbia na kutoroka, kwa sababu kwamba waliona kwamba katika jamaa huyo mdogo kulikuwako imani katika Mungu Yule aliyeweza kubadilisha maumbile yote, afanye lolote Yeye alilotaka kufanya, wakati mwanadamu angeliamini Neno Lake. Hakika. Ninaamini kilikuwa ni kitendawili.

<sup>82</sup> Musa, mtu mkuu wa kijeshi aliyejaribu kuikomboa Israeli, na hakufanikiwa. Alitaka kuwaangamiza Wamisri. Alimwangamiza mtu mmoja, naye akaingia katika shida juu yake, akilifanya kwa mapenzi yake mwenyewe. Lakini basi alichukua fimbo, fimbo kavu ya kale kutoka jangwani, na kuliua jeshi zima. Amina. Kama hicho si kitendawili, sijui ni kwa nini. Wakati alipoinua hiyo fimbo juu ya bahari, na kuiagiza bahari kujifunga; na akaizamisha Misri, taifa zima, wakati mmoja, kwa fimbo mkononi mwake. Amina.

<sup>83</sup> Kilikuwa ni kitendawili, jinsi alivyowaongoza Israeli kupitia nyikani, na kwa miaka arobaini. Ndipo walipotoka, hapakuwapo na mtu mnyonge miongoni mwao. Hicho ni kitendawili. Naam, bwana. Ilikuwa ni mtu mkuu jinsi gani, yale Mungu aliyomfanyia, kwa sababu alimwamini Mungu! Kilikuwa ni kitendawili. Naam, bwana.

<sup>84</sup> Kilikuwa ni kitendawili, wakati Mungu alipomchagua mtu mmoja mdogo, jina lake Mikaya, mbele ya manabii mia nne waliofunzwa vizuri wa Israeli, kwa sababu mtu huyu alikuwa tayari kudumu na Neno la Mungu wakati upinzani wote ulikuwa dhidi yake.

<sup>85</sup> Wakati hao mia nne waliposema, “Aa, kwea!” Alimwambia Ahabu na Yehoshafati, “Kwea, Bwana yu pamoja nawe. Ndio kwanza tupate ufunuo. Bwana yu pamoja nawe. Kwea, utawasukuma watoke nchini mwetu, kwa sababu ni yetu. Mungu alitupa. Yoshua aliigawa nchi, na hii ni mali yetu. Na hao hapo Wafilisti huko juu, wakila mahindi kutoka mashambani mwetu. Mbona, imebainika kabisa, ufunuo wetu ni wa kweli.”

<sup>86</sup> Halafu jinsi Mungu alivyomchagua mtu mdogo kama Mikaya, ambaye hakuweza hata kuingia katika shirika hilo, bali alipanda huko juu akiwa na Neno la Bwana. Ndipo akasema, “Kwea, bali niliwaona Israeli wakitawanyika kama kondoo wasio na mchungaji.” Ilikuwa ni kitendawili, jinsi Mungu angemsimamisha maskini mtu mdogo asiyetambulikana huko nje katikati ya kundi zima kubwa la manabii mia nne, la manabii wa Israeli, manabii wa Kiyahudi wakisimama pale wakitabiri uongo. Mikaya alijuaje alikuwa sahihi? Kwa sababu alikuwa sawa na Neno. Eliya alisema jambo lile lile lingetukia; naye angewezaje kubariki kile Mungu alikuwa amelaani? Ilikuwa ni kitendawili, bali Mungu alilifanya litimie. Hakika ilikuwa.

<sup>87</sup> Ilikuwa ni kitendawili; wakati maskini mvulana mdogo, aliyeonekana mwoga akiwa na maskini vishungi saba vya nywele vikining’inia chini kichwani mwake, na labda ufundo wa utepe ndani yake, nijuavyo mimi, kama maskini mwoga mdogo. Jina lake lilikuwa Samsoni. Na wakati simba, uzito wa yapata ratili mia tano, labda, simba alipomngurumia na kuja kumshambulia, basi alinyosha mikono yake akamrarua simba huyo vipande-vipande. Amina. Lakini waona kilichotukia? Roho wa Bwana alimjia, kwanza.

<sup>88</sup> Hilo ndilo linalosababisha kitendawili. Hilo ndilo. Kitendawili kama hicho kingeuwasha moto uwanja huu wa michezo, usiku wa leo, kwa utukufu wa Mungu. Kama upendo wa Bwana ungeruhusiwa kuwajilia watu, basi wangeomba. Kitendawili, kweli. Naam.

<sup>89</sup> Ambapo Samsoni alimwua yule simba, kwa mikono yake mitupu, akampasua; mvulana mdogo, mwogamwoga mwenye vishungi saba vya nywele vikining’inia chini mgongoni mwake.

<sup>90</sup> Ilikuwa ni kitendawili hapo alipochukua mfupa wa taya la nyumbu, na kuviponda vichwa elfu moja vya Wafilisti. Wakati, hizo kofia kubwa za chuma na deraya kubwakubwa, kwenye shaba zenye uzito wa labda ratili mia moja, ama karibu yake, ngao kubwakubwa na kadhalika, mikuki, watu waliofunzwa vizuri, na kofia ya chuma yenye unene wa kadiri inchi moja na nusu, ya shaba, iliyofika chini na kujikunja juu, na ni nyuso zao tu. Basi Samsoni akasimama pale akiwa na mfupa huu wa taya la nyumbu, ulikuwa umekaa pale nje labda kwa muda wa miaka arobaini, hamsini... [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Jangwani, kavu. Vema, pigo moja dhidi ya kipande

cha chuma kama hicho lingaliutawanya katika vipande milioni moja. Lakini alisimama pale, hilo ndilo jambo pekee, aliagizwa kupiga vita na kuiteka nchi hiyo. Alilelewa na kuzaliwa apate kuliua taifa hilo. Haleluya!

<sup>91</sup> Laiti kanisa lingetambua tu ni kwa nini mpo hapa! Laiti kanisa la Kipentekoste lingetambua tu ni kwa nini mpo hapa! Uwakilisho wenu ni upi? Ni kwa nini mlitoka kwenye vitu hivi kusudi muwe kile mlicheo?

<sup>92</sup> Alijua sababu ya yeye kuzaliwa. Alijua mahali aliposimama. Kitu alichokuwa nacho mkononi mwake hakikuleta tofauti yoyote. Alisimama pale, na wakati hao Wafilisti wakija. Na pigo hilo kali sana, la maskini kibushuti hicho kilichosimama juu ya mwamba, kipate kufika juu ya vichwa vyao. Wakati walipokimbia huko juu, angemtanga mmoja upande mmoja, na mmoja huo mwingine. Nao hao hapo elfu moja wamelala, wakiwa maiti pale. Ilikuwa ni kitendawili, jinsi ambavyo taya hiyo, ya nyumbu ilivyostahimili. Kilikuwa ni kitendawili, jinsi ambavyo kipande hicho cha mfupa mwepesi kuvunjika kingevunjilia mbali kofia hizo nzito za shaba na kuwaua hao Wafilisti, elfu moja ya hao. Naye angali alisimama pale amekishika mkononi mwake, kikiwa kizuri tu kama kilivyokuwa hapo alipokiokota. Kilikuwa ni kitendawili. Amina na amina!

<sup>93</sup> Angali ni yule yule jana, leo, na hata milele. Angali ni Mungu yule yule, kwa mtu yeyote aliyeitwa kulichukua Neno la Mungu. Mungu atasimama pamoja naye kama hatakuwa mwoga. Samsoni angaliweza kutoroka, bali hakufanya hivyo. Kweli.

<sup>94</sup> Kilikuwa ni kitendawili, hapo Mungu alipomwita Yohana Mbatizaji, mwana wa kuhani, kutoka kwenye shule kubwa ya makuhani, seminari kubwa. Kwa nini hiyo haikufuatia? Ambapo, ilikuwa ni desturi kwamba watu wayafuate mapokeo ya baba zao. Mbona, ilikuwa ni kitendawili, wakati Mungu alipompeleka Yohana nyikani, kumwambia kile Masihi angekuwa, kumwambia kile ishara ya Masihi ingekuwa, jinsi ambavyo angeitambua. Badala ya kwenda shuleni, kujifunza kile Masihi angekuwa; Mungu alimpeleka nyikani, kumwambia kile Masihi angekuwa. Ilikuwa ni kitendawili kikubwa, kwa hao watu katika siku hiyo. Naam.

<sup>95</sup> Wakati kuzaliwa na bikira kulipotukia, hicho kilikuwa ni kitendawili; jinsi ambavyo Mungu, kusudi ajitambulishe Mwenyewe kwa mwanadamu, alifanyika mwanadamu. Jinsi ambavyo Mungu, yule Roho mkuu...Mungu, kwangu mimi, alikuwapo awali; hakukuwako hata na nuru, hakukuwako na kimondo, hakukuwako na a—a—a—atomu, hakukuwako na molekuli, ha—ha—hakukuwako na chochote, na kila kitu kilikuwa ni Mungu. Naam, hivyo ndivyo Yeye alivyo mkuu. Ametoka Umilele, kupitia Umilele. Daima alikuwa ni Mungu. Daima atakuwa ni Mungu. Na jinsi ambavyo mkuu wa Uzima

wote alivyofanyika chembechembe ndogo hai katika tumbo la uzazi la mwanamke, kusudi apate kuitimiza sheria Yake Mwenyewe, kuilipa adhabu ya sheria Yake, mauti; jinsi ambavyo Mungu alidhihirishwa katika mwili, jinsi ambavyo Mungu mkuu wa Mbinguni alivyobadilisha sifa Yake, akaacha kuwa Mungu, apate kuwa mwanadamu, kupitia kuzaliwa na bikira, hakuna mtu awezaye kulelewa.

<sup>96</sup> Sayansi leo hii haiwezi kuwaambia jinsi kuzaliwa na bikira kulivyokuwa, bali Mungu alilifanya. Alikuwa. Hakuna aliyeweza; kila mtu alizaliwa kwa kujuana kimwili. Kama vile ninii... mtu mmoja ni kama tu hao wengine, hakuna mtu aliyeweza kumsaidia mwenzake. Sote tulikuwa katika taabu. Ndipo basi Mungu Mwenyewe akashuka chini na akazaliwa, sio kwa Myahudi, si kwa Mmataifa, bali Damu Yake ilikuwa ni Mungu. Damu hutokana na jinsia ya kiume. Katika kisa hiki, ilikuwa ni Mungu, Mungu muumba, aliumba chembechembe ya Damu katika tumbo la uzazi la Mariamu, na akajijengea Mwenyewe maskani ambamo Mwenyewe alishuka akaishi ndani yake.

<sup>97</sup> “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Neno lenyewe *Kristo* linamaanisha “Aliyepakwa Mafuta.” Loo! Yeye alikuwa ni Mungu, Mungu katika utimilifu Wake alikaa ndani Yake. Amina. “Na ndani Yake mlikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili.” Hicho kilikuwa ni kitendawili. Liliwashtusha sana watu katika siku hizo, “Wewe ukiwa ni mwanadamu, unajifanya Mwenyewe Mungu.” Lingali linawashangaza. Lakini ni vile vile tu, kingali ni kitendawili kile kile kikiendelezwa. Yeye alikuwa Mungu. Angali ni Mungu. Daima atakuwa ni Mungu. Naam, bwana. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Naam, bwana.

<sup>98</sup> Huko kuzaliwa na bikira kulikuwa ni fumbo kwa watu, wasingeweza kukuelewa, kama tu Kuzaliwa upya kulivyo leo hii. Kuzaliwa upya ni siri kwa watu. Hawawezi kukuelewa. Hawajui unalomaanisha. Wamekudunisha, wakakudhalilisha, wakisema, “Vema, kwa sababu tu unaamini jambo fulani.” Pepo wanaamini jambo lile lile, na kutetemeka. Si kile unachoamini; ni kile hasa Mungu amefanya. Kuzaliwa upya ni kuzaliwa. Kulikuwa ni kupya. Kulikuwa ni kitendawili, hapo Mungu alipouleta Uhai mpya katika jamii ya binadamu. Kuukataa, ni utengano wa Milele. Kuupokea, ni Uzima wa Milele. Nyinyi mna...

<sup>99</sup> Uko kwenye msingi ule ule kama Adamu na Hawa walivyokuwa. Unaweza kuchukua... Kama Mungu akikuweka juu ya kitu kingine chochote, ingekuwa si haki kwa Adamu na Hawa. Kila Adamu na Hawa, usiku wa leo, anayo mema na mabaya yamewekwa mbele zao. Unaweza kufanya chaguo lako. Unaweza kulichukua Neno la Mungu ama kuliacha Neno la Mungu. Unaweza kulichukua Neno la Mungu ama uchukue kanuni zako za imani ya kimadhehebu kuhusu Hilo. Unaweza kuchukua mawazo yako ya kisasa ya kile lilicho. Unaweza



kuzaliwa mara ya pili na kujazwa na Roho Mtakatifu, ama unaweza kufanywa mkanisa, lolote unalotaka kuwa.

<sup>100</sup> “Kwangu mimi kuishi ni Kristo.” Haleluya! Ninaamini ya kwamba Mungu yule yule aliyeshuka kwenye Siku ya Pentekoste, juu ya Kanisa Lake, kama Nguzo ya Moto, na kujigawanya Mwenyewe, pamoja na ndimi zilizogawanyika, miongoni mwa watu Wake, yupo hapa usiku wa leo. Ni Mungu yeye yule Yeye alikuwa wakati huo, Yeye alivyo leo, pamoja na Roho Mtakatifu yeye yule. Ninajua ni kitendawili. Haliwezi kuelezewa. Mihemuko, kupiga makelele, kulia, na kadhalika, haviwezi kuelezewa, bali ni kitendawili jinsi Mungu anavyolifanya. Ni Mungu asiyeonekana akiishi katika mwili wa kibinadamu, akijifanya Mwenyewe aonekane, kwa kulithibitisha Neno Lake, ya kwamba, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.”

<sup>101</sup> Ilikuwa ni kitendawili, wakati mwana wa seremala, Jina lake Yesu wa Nazareti, alipochukua biskuti tano ndogo na samaki wawili, na kuwalisha watu elfu tano. Kama sivyo, ninataka kumwona mtu fulani akifanya hilo leo hii. Ninawatakeni mnielezee ni atomu ya jinsi gani Yeye aliyoachilia. Alifanya nini? Sio tu samaki, bali samaki huyo alikua, huyo samaki alikuwa na magamba, samaki huyo alisafishwa, huyo samaki alipikwa, samaki huyo alikuwa chochote kile alichokuwa, na mkate huo ulipandwa ukakua; na hayo yote akayakwepa, ndipo Mungu akambadilisha kutoka—kutoka samaki aliyepikwa akawa samaki aliyepikwa. Yeye alimkuza tu kisha Yeye akamvunja, tena Yeye akamkuza na kumvunja, na Yeye akamkuza hata akawalisha watu elfu tano. Amina.

<sup>102</sup> Utaratibu huo una maana gani: kumvunja, kumkuza; kumvunja, kumkuza; kuwalisha, kumkuza? Hilo linamaanisha Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Ni Mungu yeye yule aliyekuwako. Yeye angali ni Mkate wa Uzima kwa mtu yeyote anayeona njaa na kiu. Huwezi kuumaliza wema Wake.

<sup>103</sup> Wao wanasema, “Hatuna haja na miujiza, hatuna haja na kitendawili.”

<sup>104</sup> Yeye anangojea. Huo ndio mpango Wake. Hivyo ndivyo Yeye alivyo. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Anakungojea unyoshe mkono na kuchukua sehemu yako. Unaogopa kufanya hivyo? Unaona ni afadhali ushuke uende mtoni na kujivulia samaki, na kujaribu kumpika na kumkaanga katika namna fulani ya mafuta ya nguruwe mwitu ama kitu fulani, ama unaona ni afadhali umchukue jinsi Mungu alivyo naye? Nyosha tu mkono kwa imani, na useme, “Yesu, yeye yule jana, leo, na hata milele! Ninadai, Bwana, ninakuamini Wewe. Weka ndani yangu hicho chakula, nguvu, imani ninayohitaji.” Angalia uone litakalotukia. Kwa moyo mwaminifu, Yeye atashibisha kila njaa. Atafanya hivyo.

<sup>105</sup> Yesu alikuwa ni . . . alifanya ninii . . . alikuwa na kitendawili, hapo Yeye alipowalisha watu elfu tano, kwa samaki watano, na—na kisha wakaokota vikapu viwili vilivyojaa, ama vikapu kadhaa vilivyojaa, baadaye.

<sup>106</sup> Ilikuwa ni kitendawili, wakati Mtu mwenye miguu kama niliyo nayo na uliyo nayo wewe, juu ya ziwa kama Ziwa Michigan hapa nje, wakati dhoruba zilipoingia, na yale mawimbi meupe labda yalikuwa . . .

<sup>107</sup> Vema, kama uliwahi kuwa kule na kuona vile hizo dhoruba zinavyoshuka, zingali zinafanya hivyo, kote kule Galilaya, na karibu inaonekana kana kwamba zitavuta maji chini ya bahari ziikaushe. Wakati hizo zinaposhuka kupitia pale, hizo pepo zikivuma vikali, na kuanza kufagia, nayo mawimbi meupe yakikitikisa hicho chombo hata matumaini yote yakatoweka. Na juu ya bahari hiyo, ambapo walikuwa wakipiga makasia, tangu kupiga makasia kuanzia yapata saa kumi alasiri, ningesema, mpaka kwenye mkesha wa (mwisho) nne, yapata saa tisa ama kumi asubuhi. Ni mbali kiasi gani walikuwa wamepiga makasia kuivuka bahari! Nao walimwacha Yeye ng'ambo ya pili. Amina.

<sup>108</sup> Basi kwenye mkesha wa nne, Huyu hapa anakuja, akitembea juu ya mawimbi. Hicho kilikuwa ni kitendawili. Angewezaje kujifanya mwepesi kutosha? Angewezaje kuyakanyaga mawimbi hayo, na kukanyaga wimbi moja baada ya lingine? Hayo mawimbi makubwa yakija, Yeye angeenda moja kwa moja juu ya moja, kisha ashuke aingie jingine, moja kwa moja juu ya moja, bila tone la maji juu Yake. Akaja, akitembea juu ya mawimbi! Nielezee hilo, nawe huwezi. Ilikuwa ni kitu gani? Kilikuwa ni kitendawili, kabisa.

<sup>109</sup> Kilikuwa ni kitendawili, wakati Petro, ambaye Yeye hakuwa amemwona maishani Mwake, jina lake lilikuwa ni Simoni, alitembea akaja katika Uwepo wa Yesu Kristo, kwa sababu ndugu yake Andrea alikuwa amemwambia Huyu alikuwa ni Masihi. Basi wakati Yesu alipomwangalia mtu huyo usoni, kwa mara ya kwanza Yeye aliyopata kumwona, na kusema, “Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona,” hicho ni kitendawili. Kama sicho, uniambie jinsi Yeye alivyolifanya. Ilikuwa ni kitendawili.

<sup>110</sup> Kwa nini? Kwa sababu, Yeye ni Neno. Nayo Biblia ilisema, “Neno la Mungu lina ukali kuliko upanga ukatao kuwili, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo.” Hiyo ilithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Neno, amina, “Yeye yule jana, leo na hata milele.”

<sup>111</sup> Kilikuwa ni kitendawili, wakati Filipo alipokizunguka kilima akampata Nathanaeli, na kurudi kumleta katika Uwepo wa Yesu, naye Yesu akamwambia mahali alipokuwa siku moja hapo kabla. Hicho kilikuwa ni kitendawili, amina, kilionyesha kwamba Yeye alikuwa ni Neno. “Tazama Mwisraeli ambaye ndani yake hamna hila.”

Kasema, “Ulinijua lini Wewe, Rabi?”

<sup>112</sup> Akasema, “Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.” Kitendawili. Amina.

<sup>113</sup> Ilikuwa ni kitendawili, wakati maskini mfanyabiashara, wa mji wa Yeriko, mkosoaji wa Bwana Yesu, alipopanda juu ya mkuyu, kujificha, apate kumwona akipita. Basi wakati Yesu wa Nazareti alipoingia, akitembea barabarani, na kusimama papo hapo chini ya ule mti alipokuwapo, kisha akainuka hapo juu na kumwita kwa jina lake, “Zakayo, shuka chini. Ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa ajili ya chakula cha mchana.” Kitendawili! Kamwe hakuwa amemwona mtu huyo, siku zote za maisha yake. Hakuwa amewahi kumwona.

<sup>114</sup> Ilikuwa ni kitendawili, wakati ambapo labda watu mia kadha, naam, labda watu elfu moja mia tano, elfu mbili wakitoka katika mji wa Yeriko, wakimdhihaki Yeye, na kumcheka, wakati Yeye alipoondoka humo mjini alasiri hiyo, ama asubuhi hiyo, hasa; wakati Yeye alipokuwa akitoka mjini, wakati watu wakimtupia mboga zilizooza. Nami naweza kumsikia kuhani akisema, “Aisee, wananiambia Wewe huwafufua wafu. Aisee, Ewe nabii, Wewe unayejiita Mwenyewe nabii! Wao, tunayo makaburi yaliyojaa hao hapa, mtu tu, mtu mzuri, kuhani kama nilivyo mimi; panda hapa juu, ukawafufue. Hebu tukuone Wewe ukiwafufua wafu.” Hata hakisikia neno moja walilosema, mmoja akivuta kitu kimoja, na mwingine kingine.

<sup>115</sup> Lakini huko nyuma mbali sana akiegemea ukuta, yadi mia mbili na hamsini hivi, maskini ombaomba mmoja alitetemeka kwenye baridi kule, pamoja na mikono ya mavazi yake, kasema, “Ee Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu,” na kumsimamisha Yeye njiani Mwake. Haleluya! Wito kutoka kwa Yoshua, sio mbali sana, sio—sio maili kumi kutoka mahali alipokuwa amesimama pale pale, ulilisimamisha jua, siku moja. Bali maskini mwombaji alimsimamisha M-w-a-n-a wa Mungu, akasimama njiani Mwake kwa imani yake, imani kama ile aliyokuwa nayo Yoshua. Amina. Kwa sababu, yeye alijua, kama Yeye alikuwa ni Mwana wa Daudi, Yeye alikuwa ni Masihi aliyedhihirishwa, na Yeye angeweza kuyafumbua macho yake. Kitendawili! Loo, jamani! Hakika, kilikuwa ni kitendawili. Naam, bwana.

<sup>116</sup> Mungu, ilikuwa ni kitendawili, jinsi Mungu angeweza kuwa mwanadamu, apate kufa. Mungu, Uzima, Uzima wa Milele, angeweza kuwa Mungu (uhai wa kawaida) apate kufa, ili kumwoko mwanadamu, kumrudisha kwenye Uzima wa Milele. Hicho kilikuwa ni kitendawili, jinsi ambavyo Mungu mkuu aliyejaza anga yote na Umilele wote angeweza kushuka na kufanyika mtu, ili apate kufa kuwaokoa wana-... Uumbaji Wake Mwenyewe. Jinsi Mungu alivyofanyika mmoja wa viumbe Vyake Mwenyewe, kuokoa, maana Yeye aliumba mwili Wake

Mwenyewe. Yehova Baba alikaa, katika utimilifu, ndani ya Yesu Kristo Mwana Wake. Yesu alikuwa ni mwili wa Mungu. Mungu aliwakilishwa katika maskani, mwili wa Yesu Kristo, na jinsi ambavyo Yule aliyeijaza anga yote na Umilele wote alifanyika Mtu mmoja. Amina. Mnaona ninalomaanisha? Hapo, na Mungu huyo angeweza kufanya hilo, ili kufa, na, loo, hicho kilikuwa ni kitendawili, chenyewe, jinsi ambavyo Yeye angeweza kujifanya Mwenyewe hivyo kusudi apatwe na mauti kwa ajili ya jamii yote ya binadamu.

<sup>117</sup> Lakini, loo, ni kitendawili cha namna gani, wakati Mtu aliyekuwa amesulubiwa, akauawa, akachomwa na mkuki mkubwa wa Kirumi, yapata upana wa inch sita ama nane, kupitia moyo wake, nayo Damu na maji yakafoka. Ndipo wakamtoa msalabani, amekufa, wakamfunga kwa—kwa kitambaa, kisha wakamlaza kaburini. Yeye alikuwa amekufa sana hata akida wa kirumi akasema Huyu amekufa, kila mtu pale alisema Huyu amekufa, mwezi ulisema Huyu amekufa, nyota zilisema Huyu amekufa, jua lilisema Huyu amekufa, dunia ilipatwa na ugonjwa wa kutetemeka, ikasema amekufa. Ndipo kwenye siku ya tatu, angeweza kufufuka kuwa hai tena, asiyeapatikana na mauti, kutoka mautini. Hicho ni kitendawili. Amina. Alisema, “Nina nguvu za kuulaza uhai Wangu chini; nina nguvu za kuutwaa tena.” Ufufuo Wake ulikuwa, ni kitendawili cha kweli cha Mungu.

<sup>118</sup> Kilikuwa ni kitendawili, cha Mungu, wakati Yesu alipowachagua wavuvi, wasio-...badala ya makuhani waliofunzwa, kuubeba ujumbe Wake. Ilionekana kana kwamba, wakati Yeye alipokuja, angewajia wale Mafarisayo wakuu na Masadukayo, na kusema, “Ndugu zangu, nyinyi ndio watu ambao kote katika nyakati mmeliweka dhehebu hili likiwa safi. Naja kuwachukua sasa. Baba zenu watawajivunia, wakati wanapoweza kuangalia chini kwenye milki za Mbingu,” ama popote walipokuwa. Nalitilia shaka. (Yesu alisema, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi.”) “Kwa hiyo basi angalia chini, waseme, ‘Vema, tungefurahi.’ Wangefurahia kujua hili. Nimekuja sasa kuchukulia mahali ninyi nyote mmelifikisha.”

<sup>119</sup> Ilikuwa ni kitendawili, wakati Yeye alimhukumu kila mmoja wao na kuwaambia walikuwa ni wa ibilisi, kisha akashuka kwenda kwenye Bahari ya Galilaya na kuwachagua wavua samaki wasio na elimu ambao hawakujua hata kuandika jina lao wenyewe, na kuwapa funguo za Ufalme wa Mbinguni, badala ya kumpa Kayafa, kuhani mkuu. Mtu angewezaje, kwa dini, ambayo imejaribu...kile walichofikiria kilijaribu, katika mapokeo yao na kadhalika, kudumisha mambo ya Mungu. Na Yeye huyu hapa anakuja na kuchagua kundi lingine, huko chini mtoni. Wakati mtu amefundishwa na kuelimishwa, na kupitia kwenye seminari na shule na kila kitu kingine, halafu Yeye anakuja moja kwa moja huku na kupuuza hayo, na kumchukua

mvua samaki asiye na elimu na anampa funguo za Ufalme. Amina.

<sup>120</sup> Kinachofanya kitendawili ni wakati mtu anapomwamini Mungu na kumchukua Yeye kwenye Neno Lake. Neno la Mungu liliunena ulimwengu ukawepo. Hilo ni jambo lile lile likupasalo kuamini, usiku wa leo, ni Neno la Mungu lililoahidiwa.

<sup>121</sup> Mwangalie maskini mwanamke yule mdogo amesimama pale kisimani. Alisema, “Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya.” Alikuwa amemwambia kilichokuwa shida yake. Akasema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Tunajua ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo hayo.” Angalieni.

<sup>122</sup> Mungu akizungumza na kahaba. Utukufu kwa Mungu! Mungu akizungumza na kahaba, amina, na kuomba fadhili, “Nipe maji ninywe.” Liwazie. Nena kuhusu kitendawili!

<sup>123</sup> Na ni kitendawili cha jinsi gani kwamba hiyo mbegu ya Uzima wa Milele, iliyochaguliwa tangu zamani kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu, ingekutana katika kitu kama hicho; kwa shauku ya mwili, jinsi ambavyo maskini mwanamke huyo mdogo, labda aliachiliwa kwenda mtaani, ndani ya moyo wake alikuwa amekusudiwa Uzima wa Milele.

<sup>124</sup> Wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa kabla ya kuwekwa msingi wa dunia, kulingana na Biblia, majina yetu yaliandikwa katika Kitabu hicho. Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba watakuja.” Itawanye tu Nuru!

<sup>125</sup> Angalia wakati Nuru hiyo ilipowaangazia hao makuhani na akili zao zote. Ni nini kilichotukia? Walisema, “Yeye ni Beelizebuli, mpiga ramli, ibilisi.”

<sup>126</sup> Akasema, “Ninyi ni wa baba yenu, ibilisi.” Hapo ndipo ilipotoka.

<sup>127</sup> Lakini wakati maskini mwanamke huyu, mtovu wa uadilifu akizungumza na Mungu, basi hiyo mbegu iliyochaguliwa tangu zamani ingewezaje kutiwa nanga katika m—mtu mchafu kama huyo? Ni kitendawili. Lakini angalieni wakati hiyo Nuru ilipoigusa. Kasema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii.” Sasa, nabii, ndipo ambapo Neno la Bwana huja, kwa nabii, mnaona. Na hiyo ilikuwa ndiyo dhambi yake, na Yeye nabii alikuwa na Neno. Kwa hiyo akasema, “Naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa tunajua ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atafanya mambo haya.”

Akasema, “Mimi Ndimi, ninayenena nawe.”

<sup>128</sup> Ndugu, aliacha ndoo hiyo, na akaondoka. Ushuhuda wake uliokoa mji wake, Sikari. Sasa hicho kilikuwa ni kitendawili, wakati Mungu, wakati Yesu alipofanya hivyo. Naam, bwana.

<sup>129</sup> Kilikuwa ni kitendawili, wakati Mungu alipomweka Roho Wake ndani ya wapentekoste, maskini wavua samaki na watu

wasio na elimu, badala ya Kayafa kuhani mkuu. Na, loo, jinsi alivyoiweka Injili Yake! Ilikuwa ni kitendawili, wakati Mungu alipoichagua njia iitwayo “uzushi, wendawazimu,” watu waliyumbayumba, na kuruka-ruka na kupiga makelele, na kutenda kana kwamba walikuwa wenye kichaa. Waliwaita “wendawazimu.” Ni kitendawili, wakati Mungu angeyapita masinagogi makubwa, mabaraza makuu ya Sanhedrin na makuhani walio na elimu nyingi, na kuchukua kundi la wavuvi wa samaki, wasio na maarifa wala elimu ambao hawakujua zaidi ya kumwamini Yeye tu na kulichukua Neno Lake, na kuona matokeo. Pia ilimpendeza Mungu kukiacha kile walichokiita kitu kitakatifu kuliko vyote ulimwenguni, ili kuchukua kundi la “takataka duni,” ilivyoitwa, na jinsi walivyokuwa wakiabudu, iliyoitwa “uzushi,” apate kufanya njia ya wokovu. Naam. Sasa, hiyo ni kweli, huwezi kuikana. Paulo alisema, “Katika njia iitwayo ‘uzushi,’ hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wangu, Mungu wa baba zetu; njia iitwayo ‘uzushi.’” Naam.

<sup>130</sup> Ilikuwa ni kitendawili, wakati ile Nguzo kuu ya Moto iliyoshuka kutoka Mbinguni, Malaika wa Bwana, Nguzo ya Moto iliwaongoza wana wa Israeli kupitia nyikani. Hicho kilikuwa ni kitendawili, iliyonena na Musa huko nje katika kichaka kilichowaka moto. Pia ilikuwa ni kitendawili. Na miaka mia nane baadaye...na kulingana na Maandiko, katika Yohana Mtakatifu 8:58, kama mnataka kujua mahali lilipo. Mkitaka kujua mahali ilipoanzia, kwanza, ilikuwa ni Kutoka 13:31. Basi ilikuwa ni kitendawili, wakati, baada ya safari hiyo yote na wakati huo wote, kwamba hapa Yesu alisema, kwamba, “Ibrahimi asijakuwako, MIMI NIKO.” MIMI NIKO alikuwa katika kichaka kilichowaka moto. MIMI NIKO alikuwa Ndiye aliyesema na Musa.

<sup>131</sup> Lilikuwa ni jambo la ajabu, ya kwamba baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Naye Sauli, maskini yule Myahudi mwenye pua iliyopindika, mgumu, na mwenye hasira kali, na hata aliwaua baadhi ya Kanisa; akiwa njiani kwenda huko Dameski, kuwakamata hao watu. Na huko chini walikuwa na nabii jina lake Anania, naye alikuwa huko chini akiwatabiria, nabii wa Bwana, akiwaambia Neno la Bwana, maana Yeye alimjia. Basi wakati Mchungaji Anania alipokuwa kule chini, akitabiri, Sauli alienda huko chini kumkamata. Na moja kwa moja katikati ya mchana, Nguzo ile ile ya Moto iliyoshuka na kuwaongoza Israeli, ilimpiga Sauli ikamwangusha chini. Nao watu wote, waliosimama karibu, wasingeweza kuiona Hiyo. Bali ilikuwa angavu sana, kwa Paulo, hata ikayapofusha macho yake kabisa. Amina. Alikuwa kipofu. Ilikuwa ni halisi sana kwake, na hao wengine wasingeweza kuiona Hiyo. Ni kitendawili. Jamani! Loo!

<sup>132</sup> Kile hisia moja za mtu mmoja zingetangaza, zingetangaza kwa mwingine. Hiyo ndiyo sababu watu wanaweza kuketi m—

mkutanoni, na kuiangalia kazi ya Bwana, na kusimama na kuondoka, na kuidhihaki Hiyo; naye huyo mwingine anashikilia Hiyo, kwa moyo wao wote. Ni kitendawili, jinsi ambavyo Mungu angewafanya watu, wa mwili ule ule. Ni kitendawili, kuona vile Mungu hufanya hilo, hata katika siku hii. Ilikuwa ni kitendawili kwa Paulo.

<sup>133</sup> Unajua, Paulo kamwe hakumwona Yesu katika mwili wa kawaida. Ilibidi aukubali ufunuo kama tu vile Petro alivyofanya. Petro kamwe hakumjua Yesu kwa mwili wa kawaida.

Yeye alisema, “Watu husema Mimi Mwana wa Adamu ni nani?”

<sup>134</sup> “Wengine wao walisema, mbona, Wewe ni ‘Musa,’ na wengine wanasema Wewe ni ‘Eliya,’ na ‘Yeremia.’”

Akasema, “Hilo silo nililouliza. *Ninyi* mwasemaje?”

Petro akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

<sup>135</sup> Akasema, “Heri wewe, Simoni, Mwana wa Yona. Mwili na damu havikukufunulia hili, ila Baba Yangu aliye Mbinguni amelifunua. Na juu ya mwamba huu, nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya Kuzimu hayawezi kulishinda Hilo.” Haya basi, kitendawili. Huku Yeye amesimama pale, na hakumjua Yeye katika mwili wa kibinadamu; bali alimjua Yeye kwa kazi Zake na ufunuo, akimwona Yeye akitimiza kile hasa Maandiko yalicho.

<sup>136</sup> Hicho ni kitendawili cha namna ile ile kinachomtoa mtu kutoka kwenye maskini kanuni fulani ya imani ya kawaida, kuingia katika Mungu aliye hai. Ni kitendawili, kuona mtu yule yule akiisoma Biblia ile ile, na kuikana Hiyo, wakati huyo mwingine ataiamini Hiyo na kukubali ushahidi wake. Naam, ni kitendawili, wakati anapoweza kuiona Hiyo ikitenda kazi juu ya jamaa huyo mwingine, hakika anapaswa kujua kwamba ni Mungu yule yule. Kanuni yake ya imani si sahihi, iwapo ni kinyume. Kama Mungu analithibitisha Neno Lake, basi kanuni yako ya imani si sahihi. Amina. Simaanishi kuwa fidhuli sana, bali hilo ni Kweli, kitendawili.

<sup>137</sup> Nilisema, “Dakika thelathini,” na ni hivyo hasa. Bado nina yapata kurasa sita za maandishi hapa. Kitendawili, mnaamini hicho? Amina, ninakiamini. Basi nitakoma.

<sup>138</sup> Hebu niwaambieni jambo fulani. Sikilizeni. Hapa wakati fulani uliopita, huko chini Kusini, ninakotoka, nilikuwa nikila aiskrimu kidogo, siku moja. Rafiki yangu mzee muuza dawa, mzee mtakatifu halisi aliyezaliwa mara ya pili, alikuwa ni mtu halisi. Sikuwa nimemwona kwa muda, nami nilikuwa nikipitia mjini, ndipo nikasimama ili kumwona. Ndipo nikaona jina lake pale juu, nami nikawazia, “Vema, pale, anafanya biashara hii hapa, na amekuwa hapo kwa miaka kadhaa.”

<sup>139</sup> Nikapanda juu, nikaingia, naye huyo hapo, ameketi pale, akiangalia chini juu ya maskini miwani yake, mwajua, na akiangalia juu ya maskini miwani yake iliyoning'inia shavuni mwake. Naye akasema, "Vema, kama si Ndugu Branham!" Ndipo akasimama, akaja akanikumbatia, kisha akaja akanipapasa. Akamwambia mwanawe, kasema, "Nenda ukatuletee ninii kidogo, aiskrimu kidogo." Tulikuwa tumesimama pale. "Ungetaka kikombe cha kahawa?"

<sup>140</sup> Nikasema, "La, bwana. Ningezungumzia pasipo kikomo, kama wangenipa kikombe cha kahawa." Nikasema, "Hunitia wasiwasi." Nikasema, "Nitakula tu aiskrimu kidogo."

<sup>141</sup> Kwa hiyo, tukatoa aiskrimu kidogo. Nao—nao wasichana walikuwa kule nyuma, na kadhalika, dukani, ndipo tukaketi na kufanya ushirika kidogo kwenye hiyo aiskrimu.

<sup>142</sup> Akasema, "Ndugu Branham, na—nataka kukwambia jambo fulani." Kasema, "Ni—nimekuwa kidogo sipendelei kuwambia watu wengine." Tukaanza kuzungumza kuhusu Bwana na wema wake. Huku maskini jamaa huyo analia, na machozi yakitiririka mashavuni mwake, naye akasema, "Na—nataka kukwambia jambo fulani." Kasema, "Hu—huenda likaonekana la kigeni kwa—kwako," akasema, "lakini naamini kwamba mtu kama wewe angelielewa."

Nikasema, "Vema, endelea, ndugu. Ni kitu gani?"

<sup>143</sup> Akasema, "Huko nyuma wakati wa kuzorota kwa uchumi," akasema, "mwanangu mwenye mvi pale alikuwa tu ni kijana mwanamume." Kisha kasema, "Tulikuwa hapa kwenye—kwenye biashara hii wakati huo," naye akasema, "bali watu walikuwa ni maskini na hawakuwa na chakula. Na kupata ununuzi, kupata dawa ama chochote kile, iliwabidi kwenda na kusimama katika foleni."

<sup>144</sup> Na wengi wenu mnakumbuka hilo. Hakika, mnakumbuka. Kusimama katika foleni, kupata kibali kidogo kutoka kwa wilaya, kwamba ungeweza kupata dawa hizi, ama kupata kitu cha kula.

<sup>145</sup> Naye akasema, "Nilikuwa nimeketi hapa, siku moja, nikisoma Biblia yangu, ndipo, ndipo," kasema, "mtu fulani akaingia mlangoni. Naye mwanangu akasimama, kijana, akaenda pale mbele." Kisha kasema, "Nilimsikia akisema, 'La, hatuwezi kufanya hivyo.'"

<sup>146</sup> Tena kasema, "Nilisikiliza kwa makini. Nikaweka Neno langu chini na kusikiliza kwa makini. Naye yule mtu akasema, 'Bwana,' akasema, 'mke wangu yuko karibu kuzimia.'" Ndipo alipoangalia, alisema alimwona huyo mwanamke akiwa karibu kujifungua mtoto; mume na mke wachanga. Basi yule kijana mwanamume akamwambia, "Alisema, 'Ni—ni—nimesimama katika foleni ile pale,' kasema, 'loo, urefu wa jengo la mji.' Kisha kasema, 'Mke wangu hawezi kabisa kusimama pale muda mrefu



zaidi.' Kasema, 'Sijui. . . nina maagizo kutoka kwa daktari, hana budi kupata dawa, mara moja.' Kasema, 'Je! utaijaza, kisha nimpeleke nyumbani, halafu nitaenda nisimame katika foleni? Nita—nitaleta hu—hundi kwa ajili yake. Kama utaninii. . .'

147 "Ndipo yule mwana, mvulana akasema, 'Bwana, hiyo ni kinyume na amri hapa. Sisi, hatuwezi kufanya hivyo.'

148 "Akasema, 'Vema, sikujua.' Kasema, 'Asante, sana, mwanangu,' akageuka aondoke."

149 Ndipo akasema, mara tu alipoanza kuondoka, mtu fulani akamwambia, chini—chini moyoni mwake, kasema, "Yusufu na Mariamu walikataliwa, wakati mmoja, pia."

150 Halafu akasema, "Nikaamka na kusema, 'Ngoja, mwanangu! Hebu kidogo!'" Kisha kasema, "Jamaa huyo akasimama. Nami nikaenda na kuchukua yale maagizo, nikarudi pale nyuma na kuyajaza; wakati akingojea, huku amemshika mkono mke wake. Naye alikuwa dhaifu sana, alikuwa tu ameegemea begani mwa mumewe."

151 Basi kasema, "Nilitoka hapo nje, nami. . ." Akasema, "Samahani inanilazimu kufanya jambo hili, bwana."

Akasema, "Hilo ni sawa."

152 "Alikuwa ameinamisha kichwa chake, nami nikamkabidhi tu." Basi alipoyaweka mkononi mwake, akasema, "Ndugu Branham, nilimwona Yesu." Kasema, "Niliyaweka moja kwa moja mkononi Mwake." Kasema, "Ndugu Branham, ilikuwa ni Yeye hapo, jinsi hasa picha inavyomwonyesha." Kisha kasema, "Ni—nisingeweza kuzungumza. Ndipo mtu huyo akageuka akaondoka jengoni."

Akasema, "Je! unaamini hilo, Ndugu Branham?"

153 Nikasema, "Ninaliamini kwa yote yaliyomo ndani yangu. Hakika."

154 Mtakatifu Martin wa Tours, kama umewahi kusoma juu ya Mtakatifu Martin, yeye alikuwa ni askari. Naye alikuwa—alikuwa ninii yake. . . alifuata nyayo za baba yake. Daima alihisi wito wa Mungu. Ila tu, nafikiri, watu wake hawakuwa wa kidini hasa. Basi siku moja alikuwa anakuja. . .

155 Ilikuwa ni msimu mbaya wa baridi kali, historia inasema. Naye alikuwa. . . Palikuwapo na maskini ombaomba aliyekaa nje langoni, naye alikuwa anakufa kwa baridi; na watu wengi, ambao wangaliweza kumlisha mzee huyo, ama kumpa nguo. Alikuwa analia, akiinua mkono wake juu. Maskini mzee mchafu tu mwenye masharafa, amekaa langoni mwa mji. Naye anasema, "Nisaidieni, mtu fulani. Na—naganda. Usiku wa leo nitakufa. Mtu fulani na anipe vazi."

156 Mtakatifu Martin alikuwa ametoa, yote aliyokuwa nayo. Alinirii tu, kama askari, alikuwa amevaa koti lake. Akasimama

kando, na kuangalia aone kama mtu fulani angempa. Watu wakaja na kuenda, na hakuna mtu angalimsaidia.

<sup>157</sup> Ndipo akaenda pale juu, akamwanguka mzee huyo. Akamhurumia. Akalivua koti lake, kisha akachukua upanga wake akalikata nusu. Akazungusha sehemu yake mabegani mwake, akaichukua nusu hiyo nyingine na akamfunika nayo huyo mzee ombaomba, ili aweze kuishi usiku kucha, akaendelea na safari.

<sup>158</sup> Watu wakamcheka, kasema, “Ni askari anayeonekana wa kuchekesha jinsi gani, amejivika nusu koti pekee.”

<sup>159</sup> Usiku huo, alipokuwa amelala kitandani, aliamka. Mtu fulani alikuwa ameingia chumbani. Akaangalia, amesimama upande wa pili wa chumba, na hapo alisimama Yesu na maskini kile kipande cha vazi alichokuwa amefunikwa. Alijua kwa hilo.

<sup>160</sup> Alikuwa ndiye yule mtu, Mtakatifu Martin, alikuwa ni mmoja wa wale watu walioshindania huko nyuma, ile Imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja. Yeye aliamini katika miujiza ya Mungu. Aliamini katika kunena kwa lugha. Aliamini Agano lote lililoandikwa na mitume. Yeye aliamini na kulishindania Hilo, mradi tu alikuwa hai, na Mungu alitenda miujiza. Alijua, hapo alipomwona maskini yule ombaomba amefunikwa kile kipande cha vazi la koti lake mwenyewe, kwamba Neno la Mungu lilitimizwa, “Kadiri mliyowatendea walio wadogo wa hawa, Watoto wangu, mmenitendea Mimi.”

Mnasema, “Huyo mtu hakuona hilo.”

<sup>161</sup> Ninaamini aliliona. Ninaamini alilipata. Ninaamini liko. Ninaamini huyo aliyemwanguka alikuwa ni Yesu. Ulikuwa ni ufunuo wa Mungu uliodhihirishwa, kwa sababu alilitekeleza.

<sup>162</sup> Nena kuhusu kitendawili, hicho hapo kimoja kinakuja. “Wakati waliokufa katika Kristo watakapofufuka, nasi tulio hai tutabadilishwa, katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua jicho, kunyakuliwa pamoja kumlaki Yeye hewani.” Naam.

<sup>163</sup> Loo, jinsi Mungu anavyolitimiza Neno Lake katika wakati huu wa kiakili! Jinsi ambavyo Yeye ni yule yule jana, leo, na hata mlele! Jinsi Yeye angali anaweza kuyatambua mawazo ya moyo wa mwanadamu! Jinsi Yeye angali anaweza kumbadilisha mtu! Na jinsi Yeye angali anaweza kulitimiza kila neno ambalo Yeye aliahidi katika siku hii! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele! Jinsi ambavyo angali anaweza kudhihirisha na kuwaruhusu kupiga picha ya Nguzo ile ile ya Moto iliyowafuata Israeli, Ile ile iliyokuwa pamoja na Bwana Yesu, Ile ile iliyokuwa kule chini pamoja na Sauli barabarani, Ile ile iliyolingia na kumkomboa Petro kutoka gerezeni! Malaika yule yule wa Mungu yupo hapa usiku wa leo, na kufanya jambo lile lile Yeye alilofanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani amedhihirishwa katika mwili wa binadamu. Kwa nini? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

164 Mnaamini katika kitendawili? Ninaamini ya kwamba Mungu anawataka watu waamini katika kitendawili. Nimepitisha wakati wangu kwa mbali. Ninaamini ingekuwa ni kitendawili papa hapa. Amina. Ninaamini ya kwamba Mungu yuko tayari na angependa kuchukua watu Wake na kujionyesha Mwenyewe. Kama angeweza tu kumpata mwanamume ama mwanamke, mvulana au msichana, kuweka chini mawazo yao wenyewe, na kufanyika mfungwa Kwake na kumwamini Yeye.

165 Yeye ni Neno Lake. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu.”

166 Na sasa Yeye yuko ndani yenu, tumaini la Utukufu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Alisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.”

167 Yeye aliahidi, katika Luka Mtakatifu, kwamba, “kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” wakati Kanisa teule, kundi la Ibrahimu, litapokea ishara kama Ibrahimu alivyopokea, nalo kundi la Lutu litapokea ishara kama Lutu alivyopokea.

168 Ni jambo la ajabu sana kwamba tumekuwa na hawa watengenezaji wote mashuhuri, akina Luther na Wesley, bali kamwe hatukupata kuwa na mtu huko nje ambaye jina lake linaishia katika h-a-m, mjumbe kwa ulimwengu. G-r-a-h-a-m, hizo ni herufi sita. A-b-r-a-h-a-m ni Abraham. Tumekuwa na akina Moody, akina Sankey, Finney, na Knox, Calvin, bali kamwe si *ham*, “baba kwa mataifa.” Tunaye mmoja sasa. Hicho ni kitendawili. Mlijua hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi angalieni, yeye anafanya vivyo hivyo hasa, kuwaita kutoka Sodoma.

169 Lakini, kumbukeni, Ibrahimu alikuwa na mjumbe kule juu kwa kundi lake, pia. Amina. Naye alifanya ishara ya namna gani, huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye hema? Kasema, “Nitakutembelea kulingana na wakati wa ahadi Yangu, kulingana na wakati wa uhai.” Na Yeye akasema, “Yu wapi mkeo, Sara?”

170 Kasema, “Yumo hemani, nyuma Yako.” Ndipo aliposema hivyo, Sara akacheka moyoni mwake.

171 Akasema, “Kwa nini Sara akacheka, akisema, ‘Mambo haya hayawezekani?’” Mnaona?

172 Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, kazi nifanyazo Mimi!” Neno la Mungu linatimia. “Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu yakae ndani yenu, ombeni yoyote mtakayo, nayo yatadhihirishwa kwenu.” Kitendawili, kuona ahadi ya Mungu... ahadi ya Mungu, ambayo imefanywa kwa muda wa miaka elfu mbili, na maadili ya kanisa yamewavuta watu yakawapeleka mbali sana. Lakini katikati ya hayo yote,

Mungu anashuka moja kwa moja na kulipasua Neno hilo moja kwa moja kurudi kanisani Mwake tena, vivyo hivyo hasa. Ni kitendawili. Je! mnamwamini Yeye?

Na tuombe.

<sup>173</sup> Kama kuna watu hapa ndani, usiku wa leo, ambao wangetaka kuona kitendawili kikifanywa juu yako, na kuubadilisha moyo wako kutoka kwa kutokuamini, hadi kwa imani katika Mungu, mwaweza kuinua mikono yenu, na kusema, “Bwana, nikumbuke, nikumbuke.” Mungu awabariki. Loo, angalieni tu hiyo mikono!

<sup>174</sup> Baba wa Mbinguni, kuna mikono mingi sana, nisingeweza kusema “Mungu akubariki,” kila mmoja, bali Wewe unawajua wote. Badilisha mawazo yao, Bwana. Loo, jalia litendeke, kitendawili. Daima kidogo wamekuwa wakiinama huku. Wameamini nusunusu, labda. Labda wengine wao hata ni wafuasi wa kanisa, lakini hata hivyo hawajawahi kukutana na wakati ule ambapo walikuwa na ule uhuru mkuu, wakaamini, na kujua kwamba kile Mungu alichoahidi, Mungu aliweza kufanya. Hata hivyo, tunakiri kuwa ni uzao wa Ibrahimu, ambaye hakisita kwa ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alipata nguvu, akimpa Mungu sifa. Sasa, Baba Mungu, ninakuomba Wewe, katika Jina la Yesu, uwarehemu.

<sup>175</sup> Ee Mungu, shuka chini miongoni mwetu, usiku wa leo, tenda kazi juu yetu na kutuonyesha ya kwamba Wewe ungali ni Mungu wa miujiza. Fanya kitendawili, Bwana, na uonyeshe ya kwamba Neno Lako lingali linaweza kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Wewe ungali ni Yeye yule aliyedhihirishwa huko nje, ambaye Ibrahimu alimwita Elohimu, Bwana Mungu, Mwumba, Yeye ajitoshelezaye kwa yote, aishiye kwa nafsi Yake. Ee Mungu, Wewe ungali ni Mungu wa Milele, yeye yule jana, leo, na hata milele, nayo Damu ya Mwana Wako imelitakasa Kanisa na kulisafisha. Kwamba, Neno, loo, laiti wangelilichukua tu Hilo pasipo kuongezea kanuni ya imani, Bwana!

<sup>176</sup> Lakini, sasa, Yeye alisema, “Mimi Ndimi Mzabibu, ninyi ni matawi. Tawi huzaa tunda la mzabibu; kwa kuwa uhai wa huo mzabibu, wa hilo tawi, unatoka kwenye mzabibu.” Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili, Bwana! Jinsi lilivyo kamilifu!

<sup>177</sup> Basi katika siku hii ya kutokuamini na ushirikina, na—na kila namna ya kanuni za imani, hata hivyo Wewe ni Mungu yeye yule aliyelisimamisha jua kwa ajili ya Yohana. Wewe Ndiwe uliyekuwa kwenye ile fimbo ambayo Musa aliinyosha juu ya bahari. Wewe Ndiye yeye yule ambaye angeweza kuwaita chawa, viroboto, vyura, chochote kilichokuwa, kwa kinywa cha Musa. Wewe ni Mungu yule yule ambaye angeweza kuweka mvua angani. Wewe Ndiwe utakayeshusha mvua ya moto kutoka angani. Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

178 Ee Bwana Mungu, utuonyeshe utukufu Wako, usiku wa leo, kwa kuokoa na kumjaza kila mtu aliyeinua mkono wake. Tujalie, Bwana. Jalia lisiwe tu ni ombi lingine la kiburi. Jalia isiwe ni njia nyingine ya kiburi ya kuinua mkono wetu, chini ya maskini ushawishi wa—wa jambo fulani. Bali jalia liwe linatoka kwenye kilindi cha moyo wao, hata watu waseme kwa sauti kuu, “Ee Bwana Mungu, umbra ndani yangu imani inayoweza kukuamini Wewe na inayoweza kukubali kila Neno, na kuitikia kila ahadi, kwa amina.” Tujalie, Baba. Ninalikabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

179 Vema, ni saa nne. Si lazima tufanye mstari wa maombi hapa juu. Tunaweza kuufanya kule nje. Je! mnaamini hilo?

180 Ni wangapi humu ndani wanaoamini ya kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, wanaoamini ya kwamba maskini mwanamke yule aliyeligusa vazi Lake kwa kidole chake wakati huo, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa na mwili, aliligusa vazi lake. Hicho hapo kitendawili. Yeye asingeweza kuuhihi, ndipo Yeye aligeuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa Mimi?” Basi mwanamke huyo asingeweza kujificha. Naye akamwambia shida zake, ndipo imani yake ikamponya.

181 Nayo Biblia inasema, leo, katika Waebrania, ya kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Ni wagonjwa wangapi wanaoamini hilo? Inua mkono wako. Vema, liaminini nyinyi, na hebu tuone sasa kama hiyo ni kweli.

182 Mnasema, “Ndugu Branham, hilo linakujaje?” Kuliadini tu Neno jinsi tu Hilo lilivyoandikwa. Usichukue uvumi wowote, kile jamaa *huyu* anachosema Hilo liko *hivi*, na jamaa *huyu* anasema Hilo liko *hivi*. Wewe liadini Hilo jinsi tu Hilo lilivyoandikwa.

183 Kama itambidi Yeye kukuhukumu jinsi Hilo limeandikwa, basi kwa nini uchukue tafsiri ya mtu mwingine kwa ajili Yake, maana hivyo ndivyo itakavyohukumiwa. Hilo tu, Hilo ndilo kigezo Chake. Yeye amelitunza Neno Lake. Halina kasoro. Hilo ni Neno hasa. Hilo ndilo tutakalohukumiwa kwalo, ni Hili, ni Neno la Mungu.

184 “Basi mkikaa ndani Yangu,” hiyo ni imani, “Neno Langu likae ndani yenu,” maana Yeye ni Neno, “basi ombeni mtakalo.”

185 Sasa wewe gusa vazi Lake, useme, “Bwana Yesu, ninaamini kwa moyo wangu wote ya kwamba tunaishi katika siku za mwisho. Ninaamini Wewe ni Mungu yeye yule aliyefanya miujiza hii yote ambayo mchungaji wetu ametuonyesha, usiku wa leo, katika Neno. Ninaamini ya kwamba Wewe ni Kuhani Mkuu. Bwana, jalia niguse vazi Lako. Basi Wewe nena kupitia ndugu huyu, na—na anadai kwamba Wewe husema kupitia kwake. Na, halafu, yeye hanifahamu, bali Wewe unanijua.” Na ndipo uone kama Yeye si Mungu yeye yule wa miujiza, na patokee

kitendawili tena, kitu kisichotafutika ambacho mwanadamu hawezi kukitambua na kukieleza.

<sup>186</sup> Je! mtaliadini? Kama atalifanya, basi tutajua itakuwa ni kitendawili. Hiyo ni kweli? Nilikuwa nikitaka kufanya mstari wa maombi; nikavutiwa sana na hilo mpaka ni—ni—nikaliacha, na wakati karibu umekwisha. Ninyi aminini. Hebu tuanze huku . . . Siwezi . . .

<sup>187</sup> Inanibidi kuwatenganisha. Hebu tuanze upande *huu* hapa. Mtu fulani upande *huu*. Ni wangapi *hapa* wanaojua ya kwamba siwajui au sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu; nanyi ni wagonjwa, mnajua ya kwamba mnataka kumwomba Mungu? Vema.

<sup>188</sup> Baadhi yenu wanaamini, chu—chukua tu hili kwa moyo wako wote. “Bwana Yesu, yeye yule jana, leo, na hata milele! Jalia nikuguse Wewe, Bwana. Imani yangu inasogea Kwako huko juu kwenye mkono wa kulia wa Mungu, aliyeketi katika Ukuu. Na Roho Wako Mtakatifu, aliyekuwa ndani Yako, yupo hapa usiku wa leo. Jalia tu niguse, kwa imani, Bwana.” Ndipo uone kama Yeye angali ndiye mwanzilishi wa kitendawili, kuyatimiza mambo ambayo hayajulikani kabisa. Iweni tu na kicho.

<sup>189</sup> Hapa, mnamwona huyu papa hapa? Ni mwanamke mweusi aliyeketi nyuma papa hapa. Anasumbuliwa na ugonjwa wa figo. Ndiyo kwanza afanyiwe upasuaji. Simjui mama huyu.

<sup>190</sup> Mimi ni mgeni kwako. Hiyo ni kweli, mama? Lakini hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini ya kwamba Mungu yeye yule ambaye angeweza kumwambia maskini mwanamke yule aliyeligusa vazi Lake kule, na—na ng’ambo ya pili ya ziwa, je! unaamini ya kwamba huyo ni Mungu yeye yule? Usingeweza kunigusa mimi, kimwili, unajua. Kwa hiyo nitaninii tu . . . Pia sikujui wewe. Kwa hiyo kuna Kuhani Mkuu, kwa sababu Yeye alisema Yeye alikuwa ndiye Kuhani Mkuu. Je! hiyo ni kweli? Nawe uamini hilo. Wakati ulipokuwa pale ukiomba ili iwe ni wewe, kitu fulani kilikugusa, na mara nikataja kuhusu hicho. Hiyo ni kweli? Sawa.

<sup>191</sup> Upasuaji huu uliokuwa nao haukuonekana kufanikiwa sana. Hupati nafuu, pia, nalo limekushtusha sana. Nawe umekuja hapa usiku wa leo kwa ajili ya kusudi lilo hilo. Ikiwa Bwana Yesu atanifunulia kwamba wewe ni nani, kama alivyomfunulia Simoni aliyekuja, ungeniamini mimi kuwa nabii Wake, mtumishi Wake? Unaamini hilo? Bibi Pigrum. Hiyo ni kweli. Sasa amini kwa moyo wako wote, uende nyumbani na uwe mzima. Utapata afya kwa sababu imani yako inakuponya.

<sup>192</sup> Mnaamini kwa moyo wenu wote? Vipi kuhusu katika sehemu *hii* iliyo hapa ndani, mahali fulani, mtu fulani anaamini?

<sup>193</sup> Mwanamume anayeketi hapa nje kwenye mwisho, anasumbuliwa na ugonjwa wa macho yake. Sijui kama yeye anajua . . . Naam, amenishika sasa. Anamhisi Roho. Naam, mnaaweza kuona ile Nuru juu ya mtu huyo? Bw. Otis, hilo ndilo

jina lako. Mimi ni mgeni kabisa kwako, lakini unahofia macho yako. Kristo anakuponya, imani yako.

<sup>194</sup> Sasa hebu mwulizeni mtu huyo iwapo nimewahi kumwona, kujua lolote juu yake, ama mwanamke huyu, ama popote pale. Hicho hapo kitendawili. Mnaamini hilo? Ni yeye yule jana, leo. Aliahidi, “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi pia mtazifanya.” Hivyo ndivyo Yeye alivyojitambulisha Mwenyewe kuwa ni Masihi. Hiyo ni kweli? Vema, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Nanyi mnajua haiwezi kuwa ni mimi. Mimi si Masihi. Mimi ni mwanadamu tu, ndugu yenu. Lakini ni Roho Mtakatifu hapa, ambaye ndiye Masihi. Huyo ndiye Kiongozi. Yeye Ndiye ajuaye. Siwajui hao watu; wanajua hilo.

<sup>195</sup> Hapa, ninataka kuwaonyesha. Yupo mwanamke mweusi anayeketi pale juu pembeni, pale juu, anayeugua ugonjwa wa kikoromeo. Uaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bibi Kelly. [Huyo dada anapaza sauti, “Huyo ni mimi!”—Mh.] Hiyo ni kweli. Vema

<sup>196</sup> Mnaamini kwa moyo wenu wote?

<sup>197</sup> Bw. Swanson huko nyuma, akiwa na ugonjwa wa wasiwasi, unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Kama unaliamini kwa moyo wako wote! Vema, unaweza kulipokea. Mungu anakuponya.

<sup>198</sup> Je! mnaliamini? Siwajui watu hao. Waulizeni kama ninawajua. Ni kitendawili.

<sup>199</sup> Hebu kidogo tu. Hii hapa Nuru hii, Hiyo imesimama juu ya mwanamke. Ninajua yeye ni nani. Ameketi papa hapa. Usijali, Bibi Collins, acha kujisumbua juu ya hilo, ukijifanya mwenyewe mgonjwa. Yote yatakuwa sawa. Mungu anaongoza. Sasa, ninamjua mwanamke huyo. Ninajua yeye ni nani. Ametoka huko chini Indiana, ama Kentucky. Ninamfahamu. Mume wake pale, ni mshiriki wa kanisa langu, yeye ni—yeye ni shemasi kule chini, mtu mwema. Lakini ile pale ile Nuru. Hivi hamwionni Hiyo moja kwa moja juu yake? Amesumbuliwa, yeye ni mgonjwa, pia anafadhaishwa na jambo fulani ambalo hajui kama alifanye au asilifanye. Kumbuka tu, acha kujisumbua, dada, itakuwa sawa. Yeye anajua yote kuyahusu. Ataongoza iwapo tu utamwacha Yeye aende.

<sup>200</sup> Amina! Yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye ni Kitendawili! Tunashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Mnaamini hilo?

<sup>201</sup> Simameni kwa miguu yenu na kulikubali, na kusema, “Bwana Mungu, naja Kwako katika Jina la Yesu Kristo, tenda kazi ndani yangu, na ulete utukufu na baraka Zako na nguvu juu yangu. Jalia kije kitendawili moyoni mwangu sasa hivi. Ninaamini. Ninaamini.” Kwa moyo wako wote, liamini.

<sup>202</sup> Inueni mikono yenu huku mnapoimba wimbo huu wa kale, “Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza.” Fungeni macho yenu. Fungeni mawazo yenu yote, na kumruhusu tu Yesu Kristo aingie ndani yenu, na kila mmoja wenu ataponywa na kujazwa na Roho Mtakatifu.

<sup>203</sup> Kitendawili kimoja, usiku wa leo, kingetia hii, kinapaswa kupawasha moto mahali hapa. Yesu Kristo yupo hapa. Ni nani anayeweza kueleza hilo? Waulizeni watu hawa, waendeeni. Mnayo majina yao na kadhalika, kwenye kanda hii. Nendeni, mkawaulize. Mnaona, sijui lolote kuwahusu. Kinafanya nini? Mungu, katika wakati huu wa kiakili . . .

<sup>204</sup> “Iko wapi mvua yoyote angani,” ilisema sayansi ya siku ya Nuhu, “iko wapi kule juu?” Mungu aliiahidi! Ikaja.

<sup>205</sup> Mambo haya yanawezaje kutukia? Sijui. Mungu aliyaahidi! Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Haleluya! Kitendawili! Nampenda, nampenda kwani alinipenda kwanza, na ameyafumbua macho yangu mapofu, hata ningeweza kuingia na kuuona Uwepo Wake na kujua ya kwamba Yeye yupo hapa. Amina na amina!

<sup>206</sup> Hebu tuinue tu mikono yetu na kumwabudu Yeye sasa tunapouimba. Utukufu kwa Mungu! Shukrani kwa Bwana Yesu Kristo, kwa ajili ya wema Wake na rehema! Mungu awabariki.





*KITENDAWILI* SWA63-0801

(A Paradox)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 1 Agosti, 1963, kwenye Kituo cha Marigold huko Chicago, Illinois, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)